# Tanzania

## Ripoti za Nchi kuhusu Shughuli za Haki za Binadamu - 2006

Imetolewa na Ofisi ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Kazi
Machi, 6, 2007

**TANZANIA**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yenye idadi ya watu wapatao karibu milioni 37, ni nchi yenye vyama vingi inayoundwa na Tanzania Bara na Visiwa vya Zanzibar.

Jamhuri hii inaongozwa na rais ambaye pia ndiye mkuu wa serikali na chombo kimoja tu cha kutunga sheria ambacho ni Bunge la Taifa. Hata hivyo ingawa Zanzibar imeunganishwa katika mfumo wa kiserikali na kichama ina rais wake, mfumo wa mahakama na sheria na imeendelea kuwa huru kwa kiasi cha kutosha. Katika uchaguzi wa rais na wabunge uliofanyika mwezi Desemba 2005, Jakaya Kikwete alichaguliwa kuwa rais na chama tawala, Chama cha Mapinduzi (CCM) kilipata ushindi wa kura nyingi kwa wabunge.

Wachunguzi waliafiki kwamba uchaguzi katika Jamhuri hii ya Muungano ulikuwa kwa kiwango kikubwa huru na wa haki Bara na Visiwani Zanzibar. Uchaguzi wa rais wa mwaka 2005 Visiwani Zanzibar ulikuwa na ushindani zaidi, ukiukwaji mkubwa wa taratibu za uchaguzi na vurugu za kisiasa.

Hata hivyo, kulikuwa na uboreshaji katika uendeshaji wa uchaguzi. Ingawaje kwa jumla madaraka ya kiraia yalidhibiti sana nguvu za vyombo vya usalama, kulikuwa na matukio ya hapa na pale ambapo vyombo vya usalama vilifanya vitendo bila mamlaka ya serikali.

Kulikuwa na matatizo yanayohusu haki za binadamu kadhaa yanayoendelea. Polisi na askari wa magereza walitumia nguvu kupita kiasi dhidi ya wafungwa au watuhumiwa, na wakati mwingine yalisababisha vifo na hivyo kutoadhibiwa kwa polisi lilikuwa tatizo; kulikuwa na ripoti zilizoendelea kutolewa kuhusu mauaji ya vikongwe waliotuhumiwa kuwa wachawi; hali za magereza zilikuwa za kikatili na zenye kutishia maisha; daima polisi walifanya upekuzi bila vibali, mara nyingi walikuwa fisadi na wakati mwingine walishindwa kuwaleta mbele ya jaji watu waliowaweka kizuizini kwa wakati walipotakiwa; mfumo wa mahakama ulijaa ufisadi katika mahakama ya mwanzo; uhuru wa kusema na pia wa vyombo vya habari kwa kiasi fulani ulizuiwa; ufisadi wa serikali uliendelea kuzagaa; mamlaka zilizuia uhuru wa wakimbizi kutembea; uonevu wa kijamii dhidi ya wanawake uliendelea; na usafirishaji haramu wa watu na ajira kwa watoto ulikuwa matatizo.

## HESHIMA KWA HAKI ZA BINADAMU

### Sehemu ya 1: Heshima ya Hadhi ya Mtu ikiwa ni pamoja na Kuepuka Uhuru wa :

**a. Upokonyaji wa maisha kidhalimu au kinyume cha sheria**

Hapakuwa na mauaji ya kisiasa yaliyofanywa na serikali au wakala wake katika mwaka huu. Hata hivyo, katika matukio kadhaa vyombo vya usalama vilitumia nguvu ya kusababisha mauti kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na mahabusu. Katika mwaka huu

viongozi (wa Haki za Binadamu) walishutumu polisi kwa kuwaua watu kadhaa kinyume cha sheria. Kwa mfano, mnamo mwezi Januari, katika viunga vya Jiji la Dar es Salaam, polisi 15 waliwapiga risasi na kuwaua wafanyabiashara ya madini watatu na dereva wa teksi wakidai kwamba watu hao wanne walikuwa waporaji. Iliarifiwa kuwa watu hao walikuwa hawakukataa kukamatwa na tume maalumu ikiongozwa na Jaji wa Mahakama Kuu ilichunguza tukio hilo na kugundua kuwa watu hao hawakuwa waporaji. Mamlaka iliwafungulia mashtaka ya mauaji askari polisi wote hao 15. Hadi kufikia mwisho wa mwaka, kesi hiyo ilikuwa ikisubiri uamuzi.

Mnamo mwezi Machi, kulingana na taarifa za maofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, polisi mjini Mwanza walimtesa na kumuua dereva mmoja wa teksi aitwaye Christopher Samson wakati akiwa mahabusu baada ya kukamatwa kwa kudaiwa kwamba alishiriki katika wizi kwa kutumia silaha. Kamanda wa Polisi wa Mkoa aliwahoji mapolisi waliohusika na baadaye walikamatwa. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka hapakuwa na taarifa nyingine kuhusu kesi hii.

Tarehe 6 Mwezi Juni, ilidaiwa kuwa askari sita wa Magereza walikuwa wamemuua mfungwa, Eladius Stanslaus katika gereza la Kimbiji, Wilayani Temeke katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Temeke aliahirisha kesi hii kwa sababu uchunguzi ulikuwa haujakamilika siku ya kesi. Hakuna taarifa zaidi iliyopatikana kufikia mwishoni mwa mwaka.

Tarehe 16 Mwezi Julai, Mamlaka katika Mkoa wa Shinyanga iligundua maiti ya mwanaume katika Mahabusu ya Polisi katika Kijiji cha Kagongwa. Kutokana na taarifa ya vyombo vya habari, askari Magereza alimpiga mfungwa na kumuua katika gereza la Kisongo, Mkoani Arusha.

Hapakuwa na ripoti za utafiti uliokuwa ukifanyika kuhusu mauaji kadhaa au madai ya mauaji yaliyofanywa na polisi au viongozi wa Magereza mwaka 2005.

Kulikuwa na mauaji kadhaa yaliyokuwa hayajakatiwa kesi tangu mwaka 2004. Yalihusisha pia mauaji ya mwezi Julai ya Selemani Juma Mousi yaliyofanywa na polisi na kifo cha kijana mdogo wakati wa uchaguzi kwa madai ya kuwa matokeo ya polisi walipotumia nguvu nyingi. Katika tukio hili la mwisho viongozi wa chama cha upinzani walishutumu kwamba polisi alikuwa hawapelelezi. Hapakuwa na ripoti ya maendeleo ya upelelezi kuhusu mauaji ya mwanafunzi anayedaiwa aliuawa na askari wa kikosi cha kuzuia ghasia; viongozi waliwasilisha ombi la uchunguzi rasmi kufanywa mwezi Agosti 2005 lakini kulikuwa na taarifa kwamba mtuhumiwa alikwisha kuhamishiwa Bara. Ingawa mwezi Agosti 2005 viongozi waliwasilisha ombi uchunguzi rasmi ufanywe kuhusu mauaji ya mkaguzi wa majengo Arusha yaliyotuhumiwa kufanywa na polisi, hadi kufikia

mwishoni mwa mwaka hapakuwa na taarifa zaidi. Hapakuwa na maendeleo kuhusu mauaji ya mfanyakazi wa Shirika lisilo la Serikali huko Wilayani Ngara na watu wasiojulikana waliokuwa na silaha; na pia hapakuwa na ripoti kwamba viongozi walikuwa wakifuatilia tukio hilo (tazama sehemu ya 4).

Vifo kutokana na hasira za makundi ya watu viliendelea vikiwa ni pamoja na kuua kwa kupiga mawe, vipigo, kukatakata kwa mapanga na kuchoma moto lakini vilipungua kwa idadi kutokana na usambaaji wa kampeni za serikali kuzuia mauaji kutokana na hasira za makundi. Mwezi Agosti kundi la watu wenye hasira walimchoma moto Saidi Sudi ambaye baadaye alikufa kutokana na majeraha aliyopata. Mwezi Desemba kundi la watu wenye hasira liliwanyonga majambazi wawili ambao hawajulikani mkoani Shinyanga. Kuwatia hatiani wahusika katika matukio kama haya ilikuwa vigumu; viongozi walibainisha kwamba mara nyingi ilikuwa vigumu kuwashawishi mashahidi kutoa ushahidi wao. Hata hivyo, mapema mwezi Julai Mahakama kuu ilihukumu watu watatu wauawe kwa kosa la kumuua Ernest Kikoti kwa mauaji ya kundi lenye hasira katika kijiji cha Nyamvisi katika Mkoa wa Morogoro. Upande wa mashitaka uliwashitaki washitakiwa kwa kosa la kuchochea kundi la watu kumuua Kikoti.

Mauaji ya watu wanaotuhumiwa kuwa wachawi yaliendelea. Imani ya uchawi iliyoenea ilisababisha mauaji ya watu wengi sana waliodhaniwa kuwa wachawi na wale waliodai kuwa waliathirika, ndugu wa waathirika wenye uchungu au makundi yenye hasira. Desturi hii ambayo mwanzo ilikuwa imejikita tu katika Mkoa wa Shinyanga sasa imeenea katika mikoa mingine kutokana na uhamaji wa wafugaji kutoka Mkoa wa Shinyanga. Kwa mfano tarehe 16 Aprili watu wasiojulikana katika kijiji cha Buhanga, Mkoa wa Kagera, walimuua Bibi Kizee mwenye miaka 67 aitwaye Anna Maria, aliyetuhumiwa kwa uchawi na mjukuu wake mwenye miaka saba aitwaye Sicholesik.

Mwezi Desemba Mwema Bakari Kassan, mkazi wa kijiji cha Kiyanga katika Mkoa wa Mtwara alikamatwa na Polisi kwa kudaiwa kushiriki katika kuchoma moto nyumba tano ambazo alidhania kwamba mganga wa kienyeji alikuwa amemficha mmoja wa ndugu zake. Hadi mwishoni mwa mwaka kesi ilikwua bado katika uchunguzi. COEL imebainisha kwamba matukio haya yalikuwa ya kawaida sana katika Mikoa ya Tabora, Mwanza, Shinyanga na Kigoma.

Tarehe 28 Agosti gazeti la *The African* likinukuu takwimu kutoka Shirika lisilo la kiserikali la hapa nchini la Concern for the Elderly (COEL), liliarifu kwamba katika muongo uliopita wazee 8,500 katika Kanda ya Ziwa walikuwa wameuawa kutokana na madai ya uchawi.

Serikali iliwashitaki watu walioshutumiwa kuwaua watu waliotuhumiwa kufanya vitendo vya uchawi, lakini mashitaka

hayo yalikuwa vigumu kuyaendesha kwa vile wahusika waliofanya mauaji ya watu waliotuhumiwa kuwa wachawi walijua jinsi ya kukwepa vyombo vya utekelezaji wa sheria.

Katika mikoa miwili kulikuwa na ripoti kuwa watu waliofanya shughuli za kichawi waliwaua watoto na wanafunzi, kwa madai ya kunyofoa viungo vya mwili na ngozi na kuviuza (tazama sehemu ya 5).

**b. Utowekaji**

Hapakuwa na ripoti za utowekaji uliochochewa kisiasa

**c. Utesaji na Vitendo vya kikatili, vya kinyama au Udhalilishwaji au Adhabu**

Katiba na Sheria vinazuia vitendo kama hivyo. Hata hivyo, kuliendelea kuwepo ripoti kwamba polisi waliwatesa watu, kuwatishia au vinginevyo kuwasumbua wahalifu watuhumiwa na wafungwa katika mwaka huu. Vipigo na viboko zilikuwa ndizo njia zilizotumika sana. Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari; ni idadi ndogo zaidi ya polisi ilishutumiwa kwa kuwatukana wafungwa katika mwaka huu, kutokana na polisi wahalifu kushitakiwa mara nyingi zaidi.

Jitihada za viongozi wa Jiji kuwaondoa wachuuzi wa bidhaa mitaani kutoka maeneo makuu zilisababisha kutokea majeruhi. Tarehe 9 Machi, vikosi vya askari wanamgambo viliwajeruhi wachuuzi wa bidhaa mitaani wakati wa kuwaondoa mitaani katika Jiji la Mwanza. Tarehe 10 Machi vikosi vya askari wanamgambo vilipambana na wachuuzi wa bidhaa mitaani katika Jiji la Dar es Salaam, katika kutekeleza amri ya Waziri Mkuu kwa viongozi wa Jiji kusitisha kuwafukuza na kuwapa miezi sita wafanyabiashara hao kujiandaa. Mwezi Oktoba baadhi ya wachuuzi wa bidhaa waliokataa kuhamia katika maeneo maalumu yaliyotengwa walijeruhiwa baada ya kupambana na wanamgambo.

Tarehe 26 Agosti, gazeti la *The Guardian* liliarifu kwamba kutokana na kipigo cha askari polisi wa Zanzibar ilibidi Said Awadhi aondolewe jicho lake la kushoto hospitalini. Awadhi aliwashutumu askari wa doria katika eneo la Mpendae kumpiga pasipo sababu yoyote. Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa eneo hilo alisema kwamba suala hili lingaliweza kuchunguzwa kama mwathirika angalikuwa amearifu jambo hilo ofisini mwake; hapakuwa na dalili kwamba viongozi walikuwa wakifuatilia suala hili.

Tarehe 27 Agosti, Waziri wa Usalama wa Raia alitangaza kwamba Mkuu wa Jeshi la Polisi alikuwa ameanza kuwaondoa wahalifu katika jeshi la polisi na kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa askari polisi. Inawezekana, majeraha yaliyokuwa yametokea kwa maofisa wawili wa polisi wakati walipokuwa

wakikamatwa mwezi Julai yalikuwa ni mojawapo ya sababu zilizokuwa zimechochea hatua hiyo.

Tarehe 6 Februari, Lucas Omahe Galani alihukumiwa kifungo cha miaka 10 jela kwa kumshambulia ghafla Mgombea wa Urais wa CCM, Jakaya Kikwete, wakati wa mkutano wa hadhara wa Oktoba Jijini Mwanza.

Mnamo mwezi Septemba 2005 serikali iliunda tume ili kuchunguza madai ya kuwapo vitendo vya utesaji mbaya ambamo Maofisa Magereza Waandamizi walihusika Wilaya ya Geita katika mkoa wa Mwanza. Maofisa hao walishutumiwa kwa kuwatesa, kuwapiga na kuwalawiti wana sungusungu wawili ambao ni walinzi wa jadi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka kesi hiyo ilikuwa bado mahakamani.

Mara chache Maofisa wa serikali za mitaa na mahakama walitumia viboko kama adhabu kwa watoto wahalifu na watu wazima, na walimu na viongozi wa shule walitumia viboko na adhabu za aina nyinginezo za kutandika viboko wanafunzi (tazama sehemu ya 5). Kwa mfano, mnamo mwezi Mei 2005 Mahakama moja ya Hakimu Mkazi huko Arusha ilimhukumu mfanyabiashara maarufu kwenda jela na kupigwa viboko 12 kwa kosa la kumbaka mtumishi wake wa nyumbani. Utumiaji wa viboko ulizidi kupungua katika kipindi cha mwaka huu kutokana na juhudi za serikali kuufikia umma ...... hasa Wizara ya Elimu..... na vyombo vya habari.

Kulikuwa na ripoti chache zaidi katika kipindi cha mwaka huu kuhusu askari kuwapiga raia. Hata hivyo, mnamo mwezi Machi askari wa Mgambo na Polisi wa Manispaa waliokuwa wakiwafukuza wapiga debe wa mabasi (yaani vijana ambao hujidai kuwaelekeza abiria kuingia katika mabasi lakini mara nyingi kwa kujipatia malipo kutoka kwa madereva), waliwajeruhi takriban watu 20 katika vituo vya Mwenge, Kariakoo na Tandika vya Dar es Salaam. Inadaiwa Polisi waliwapiga wapiga debe hao na kuwalazimisha kulala katika madimbwi ya maji machafu ya mvua.

Kufikia mwishoni mwa mwaka hapakuwa na taarifa zaidi kuhusu matukio mawili ya vipigo ambapo askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) waliwashambulia wachuuzi wa bidhaa wa mitaani na kutumia nondo dhidi ya Wanakijiji cha Boko, Wilayani Kinondoni.

Kinyume na mwaka 2005, hapakuwa na ripoti kwamba askari Polisi walitumia nguvu nyingi kuvunja maandamano.

Tofauti na mwaka 2005 hapakuwa na ripoti kwamba polisi waliwanyanyasa kingono watu waliokuwa wamewakamata.

**Hali ya Magereza na Vituo vya Mahabusu**

Hali ya magereza iliendelea kuwa ya kikatili na ya kutishia maisha. Mwaka 2005 kiwango cha mwisho kilichowekwa kitaifa cha uwezo wa kutoa huduma ndani ya gereza kilikuwa 23,000, na idadi ya watu katika gereza ilikisiwa kuwa 46,000. Katika kipindi cha mwaka huu magereza nchini yalikuwa na wafungwa waliohudumiwa 23,968 na mahabusu waliokuwa wakisubiri hukumu walikuwa 21,017 na hivyo kuwa na jumla ya idadi ya wafungwa 44,985. Mwaka 2005 John Chiligati aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo alisema kwamba nchi ilihitaji vifaa 156 vya gereza ikilinganishwa na idadi ya vifaa 122 vilivyokuwepo. Tarehe 9 Julai aliliambia Bunge kwamba kulikuwa na msongamano katika magereza yote ya nchi nzima.

Katika kipindi cha mwaka huu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikagua zaidi ya jela 10 kufuatilia ukiukwaji wa Haki za Binadamu. Mnamo mwezi Oktoba serikali ilikiri kuwepo matatizo makubwa ya msongamano wa watu, magonjwa ya kuambukiza, uwekaji mahabusu kwa muda mrefu kabla ya kufikishwa mahakamani na kuwachanganya wafungwa watoto na watu wazima.

Wafungwa walipambana na hali ngumu za maisha na hawakupata mahitaji ya msingi ya binadamu. Asasi zisizo za serikali (AZISE) ziliarifu kwamba wafungwa walipata chakula kisichofaa kama matokeo ya viwango visivyotimia vya udhibiti wa majitaka kwa afya na usafi. Mwezi Januari, 2005 zaidi ya wafungwa 15 wa Gereza Kuu la Ukonga, Jijini Dar es Salaam walilalamika kuhusu chakula kibaya na vipigo vibaya vya askari jela. Mara nyingi uongozi ulihamishia wafungwa gereza jingine bila kuzipa taarifa familia zao.

Zahanati za jela zilitoa matibabu madogo tu, na mara nyingi marafiki na wanafamilia wa wafungwa ilibidi watoe dawa au fedha za kununulia dawa hizo. Maradhi yalikuwa jambo la kawaida na yalisababisha vifo vingi katika magereza. Kwa mujibu wa ripoti za AZISE, sababu za vifo zilikuwa magonjwa ya malaria, kifua kikuu VVU/UKIMWI, kipindupindu na magonjwa yanayohusiana na kiwango duni cha kutodhibiti majitaka kwa afya.

Mnamo mwezi Februari ili kudhibiti uenezaji wa VVU/UKIMWI katika magereza, serikali ilianzisha vituo 12 vya Hiari vya ushauri na upimaji ili kutoa huduma katika asasi zote zinazotoa adhabu.

Kulikuwa na ripoti kwamba askari wa magereza waliwapiga na kuwafanyia vitendo vibaya vya ngono katika kipindi cha mwaka huu.

Hakuna ripoti ya uchunguzi iliyotolewa kutoka tume ya serikali inayochunguza ukamataji, uwekaji kizuizini na utesaji wa walinzi wa jadi wanasungusungu wawili uliofanywa na ofisa Magereza huko Mwanza. Kwa amri ya huyo Ofisa Magereza, wafungwa wanane waliwapiga na kuwatendea vitendo vichafu vya ngono hao watu wawili ambao ilibidi walazwe hospitali baada ya kuwekwa kizuizini.

Sheria inataka wafungwa watenganishwe kadiri ya umri na jinsi. Lakini katika hali halisi magereza mengi yenye msongamano hayakuwa na vyumba maalumu vya wafungwa wanaume, wanawake na watoto wadogo. Kulikuwa na takriban magereza 10 maalumu ya wafungwa watoto kwa nchi nzima. Serikali ilibainisha kwamba wafungwa wenye umri kati ya miaka 18 na 21 ni wafungwa watoto na iliagiza magereza kuwatenganisha na wafungwa watu wazima nyakati za usiku. Mahabusu waliwekwa pamoja na wafungwa waliokwisha kuhukumiwa na waliruhusiwa kupokea chakula kutoka nje.

AZISE za hapa nchini, Mashirika ya Kimataifa na watazamaji wa kidiplomasia waliruhusiwa kukagua hali za magereza wakati wa kipindi cha mwaka huu. Kwa mfano, tarehe 8 Mei, Chama cha Msalaba Mwekundu kilitembelea Gereza la Segerea Jijini Dar es Salaam. Kamati ya Kimataifa ya Chama cha Msalaba Mwekundu (ICRC) iliwatembelea wafungwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Rwanda, Jijini Arusha. Serikali iliruhusu Ofisi ya Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa (UNHCR) kutembelea magereza walimo wakimbizi mjini Dar es Salaam na Magharibi. Kamati hiyo ya Kimataifa ilivitembelea vituo viwili huko Zanzibar mwezi Desemba lakini hawakukagua vifaa kwa wafungwa wa nchini wakati wa kipindi cha mwaka huu.

**d. Ukamataji watu Kiholela na Kuwatia kizuizini**

Katiba inazuia ukamataji watu kiholela na kuwatia kizuizini. Hata hivyo, mambo haya yalikuwa matatizo.

Nafasi ya Polisi na Vyombo vya Usalama

Jeshi la Polisi la taifa chini ya Wizara ya Usalama wa Rais, lina jukumu la kwanza la kudumisha sheria na utaratibu. Kikosi cha Kuzuia Ghasia (FFU) ni sehemu ya Jeshi la Polisi. Vikundi vya doria vya jadi vya Sungusungu viliendelea kusaidia Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na kambi za wakimbizi. Polisi hawakuwa na jukumu la kuwasimamia Sungusungu ambao walifanya shughuli zao na viongozi wa Serikali za Mitaa. JWTZ, chini ya Wizara ya Ulinzi lina jukumu la ulinzi nje ya nchi na pia lina majukumu fulanifulani ndani ya nchi.

Jeshi la Polisi liliendelea kutopata fedha za kutosha na hivyo kutokuwa na ufanisi. Matumizi ya nguvu nyingi kupita kiasi, ufisadi wa polisi na uvunjaji wa sheria bila woga yalikuwa matatizo makubwa.

Mara nyingi wananchi walinung'unika kwamba polisi hawakuwa wepesi kuchunguza makosa ya uhalifu na kuwashitaki wahalifu. Askari Polisi ingawa wao si wanasheria ndio walikuwa washitaki katika Mahakama za Mwanzo. Wataalamu wengi wa sheria walikosoa utaratibu huu, ambao ilidaiwa uliwezesha polisi kupinda ushahidi katika kesi za jinai na wakati mwingine ukasababisha baadhi ya kesi kuondolewa mahakamani. Kwa mujibu wa ripoti za AZISE, kulikuwa na matukio ambapo polisi walipoteza ushahidi na watuhumiwa waliokuwa na uwezo wa kutosha walifaulu wasishitakiwe kwa kuwahonga maofisa wa polisi. Vilevile polisi walitumia kitisho cha kukamata watu holela kujipaia fedha. Jumuiya zilitambua hali ya jumla ya kutokuwepo na ulinzi katika kipindi cha kuongezeka uhalifu na watu waliotumia silaha. Kukosa imani kwa Jeshi la Polisi na pia kwa mfumo wa mahakama vilichangia katika makundi ya watu wenye hasira kufanya uamuzi wao wenyewe katika kipindi cha mwaka huu. mifumo ya taratibu za ndani katika mpangilio wa polisi ilikuwapo kuchunguza uvunjaji wa sheria uliofanywa na polisi lakini mbali na uboreshaji uliofanywa, uendeleaji wa tabia mbaya za polisi ulionyesha kwamba mifumo hiyo ilikuwa haitumiki kwa dhati.

Katika kipindi cha mwaka huu kuliendelea kuwepo kwa ripoti nyingi za vyombo vya habari na manung'uniko kutoka katika makundi ya raia na wananchi kwa jumla kuhusu ufisadi wa polisi. Kitengo cha kuzuia ufisadi kilitoa taarifa ya manung'uniko mengi ya watu ambapo kililihusisha Jeshi la Polisi na viongozi wa mahali husika. Mwezi Julai, Mkoa wa Kagera uliongoza katika orodha ya manung'uniko ya ufisadi ukiwa na manung'uniko 558 yaliyokuwa yameandikwa katika mwaka 2005. Mwezi Novemba vyombo vya habari vilitoa taarifa kwamba dawa za kulevya zenye thamani ya maelfu ya dola ziliibwa zikiwa katika ulinzi wa polisi kutoka Kitengo cha Kuzuia dawa za kulevya kilicho katika Wizara ya Mambo ya Ndani, Dar es Salaam. Kamanda wa Kitengo hicho alibadilishwa na askari wawili walikamatwa. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka kesi ilikuwa ikisubiri uamuzi.

Mwezi Januari Rais Kikwete aliielekeza Wizara ya Usalama wa Raia na maofisa waandamizi wa Polisi kumchukulia hatua za nidhamu polisi yeyote ambaye hakuwa na "msimamo wa maadili" Mwezi Machi Jeshi la Polisi lilianzisha uchunguzi wa sajenti mmoja wa Polisi aliyedaiwa kumiliki mali isiyolingana na kipato chake. Mkuu wa Polisi wa Mkoa, Alfred Tibaigana alisema polisi huyo angefukuzwa kazi kama ingethibitishwa kuwa ana hatia. Katika kipindi cha mwaka huu, Tibaigana alisema pia kwamba ofisa mwingine wa polisi aliyekuwa akidaiwa kushirikiana na raia kuiba mali za nyumbani pia angefukuzwa kazi kama ingethibitishwa kuwa ana hatia.

Katika kipindi cha mwaka huu jeshi la polisi liliendesha semina za mafunzo kuhusu ukachero wa upelelezi, haki za binadamu, uharakishaji wa upelelezi, ukamilishaji wa kesi za jinai na jinsi ya kuwachukulia wanachama na viongozi wa vyama vya upinzani. Sheria inavipa hadhi ya kisheria vikundi vya jadi vya Sungusungu na vikundi vya kuzuia uhalifu vijijini. Serikali za Mitaa huteua wanachama kwa kusaidiana na watu binafsi majumbani ambao huamua nani kati yao atajiunga na ulinzi wa Sungusungu. Walinzi wa Sungusungu waliendelea kufanya shughuli zao katika maeneo ya vijijini kama vile katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza na pia katika kambi za wakimbizi, lakini bado hawakuwepo katika maeneo mengi ya vijijini. Sungusungu wana mamlaka ya kuwakamata watu, lakini hawana mamlaka ya kubeba silaha na badala yake walibeba rungu kwa ajili ya ulinzi. Sungusungu wamekosolewa kwa kutumia nguvu nyingi kupita kiasi, ikiwa ni pamoja na kutoa vipigo vikali kwa watuhumiwa ambavyo mara nyingi vilisababisha vifo. Ilikuwa ni desturi kwa wenyeji wa eneo ambamo Sungusungu walifanya shughuli zao ama kutoa kiasi fulani cha fedha kwa wanasungusungu kama hawana fedha au, kama hawakuwa na fedha, kutoa mtu mmoja wa eneo hili ili ashirikiane nao katika doria. Katika kambi za wakimbizi, zaidi ya kuwepo kikundi cha polisi wa kawaida, vikundi vya sungusungu vya wakimbizi vilifanya kazi kwa namna fulani rasmi kama vikundi vya usalama.

**Ukamataji na Utiaji Ndani watu**

Sheria inataka kwamba watu wakamatwe kwa uwazi kwa vibali vyenye ushahidi wa kutosha, na Mamlaka kwa jumla zilifuata sheria. Vilevile Sheria inataka kwamba mtu aliyekamatwa kwa kosa la uhalifu, mbali na yule aliyetiwa ndani kwa usalama wa taifa (kama ilivyoelezwa katika sheria ya kuzuia kutiwa ndani), anapaswa afunguliwe mashitaka mbele ya hakimu ndani ya saa 24 baada ya kukamatwa. Lakini katika hali halisi mara nyingi polisi walishindwa kutii masharti haya. Sheria inawapa washitakiwa haki ya kuwasiliana na mwanasheria au kuzungumza na wanandugu lakini wakati mwingine mamlaka zilikataa haki hii. Kupatikana kwa ushauri wa haraka pia kulipunguzwa kutokana na uchache wa wanasheria vijijini, kutokuwepo kwa mifumo ya mawasiliano na miundombinu na pia kutojua na umaskini kwa mshitakiwa. Harakaharaka mamlaka ziliwaarifu na walitiwa ndani kwa makosa yao. Serikali ilitoa uwakilishi wa kisheria kwa washitakiwa maskini kama ilivyofanya kwa watuhumiwa wote walioshitakiwa kwa mauaji au uhaini. Sheria hairuhusu uwezekano wa kutolewa dhamana kwa makosa ya mauaji au wizi kwa kutumia silaha na inatoa masharti magumu ya uhuru wa kutembea na kuchanganyika na watu dhamana inapotolewa katika kesi nyingine. Katika Mahakama za Mwanzo na za Wilaya, wakati mwingine hongo ndiyo iliyoamua kupatikana kwa dhamana.

Kwa mujibu wa Sheria ya kutiwa Kizuizini, rais anaweza kuamuru kukamatwa na kutia kizuizi kwa muda usiojulikana na bila dhamana, kwa mtu yeyote anayeonekana hatari kwa utaratibu wa umma au kwa usalama wa taifa. Sheria inaitaka serikali kuwaachia watu wanaozuiwa kwa mujibu wa Sheria hii, ndani ya siku 15 baada ya kukamatwa kwao au kuwaambia sababu ya kuwekwa kwao kizuizini. Pia inamruhusu aliyewekwa kizuizini kupinga mazingira yaliyosababisha awekwe kizuizini kila baada ya kipindi cha siku 90. Serikali ina mamlaka mapana ya nyongeza katika sheria hii ambayo yanawaruhusu Wakuu wa Mikoa na Wilaya kukamata na kutia kizuizini kwa muda wa saa 48 watu ambao huweza "kuvuruga utulivu wa umma." Katika kipindi cha mwaka huu sheria hii haikupingwa.

Mwezi Julai, Waziri wa Sheria na Katiba, Mary Nagu alisema kwamba mahakama za sheria zilipokea kesi za watu waliodhulumiwa zilizoonyesha kutiwa ndani kinyume cha sheria kuhusiana na uchaguzi wa mwaka 2005. Kesi tano kati ya kesi hizo zilitupwa kwa kushindwa kutimiza masharti ya kisheria. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka kesi 31 zilizobaki zilikuwa zikisubiri uamuzi mahakamani.

Tofauti na mwaka 2005, uliokuwa mwaka wa uchaguzi kitaifa, hapakuwa na ripoti za kutiwa ndani kiholela kwa viongozi wa vyama vya upinzani au wafuasi wao.

Hapakuwa na taarifa kuhusu kesi ya Abdul Rashid mkazi wa Dar es Salaam ambaye alidai kwamba alitiwa ndani kiholela aliyekamatwa mwezi Septemba mwaka 2005. Alishtakiwa kwa makosa ya kuharibu bango la Kampeni la CCM. Rashid alikataa mashitaka hayo.

Polisi waliwakamata wakimbizi kwa kuondoka kambini bila ruhusa (tazama sehemu ya 3.d)

Tofauti na mwaka 2005, hapakuwa na ripoti ya kwamba askari wa usalama wa Muungano walioko Zanzibar au wale wa usalama wa Visiwani wanaojulikana kama "vikosi", walifanya vitendo vya kuvunja haki za binadamu katika kipindi cha mwaka huu, na hapakuwa na madai kwamba tawi la CCM la Zanzibar lilishirikiana na "vikosi" kutoa mafunzo kwa kikundi cha "janjaweeed" kikundi kinachodaiwa ni cha CCM chenye lengo la kutishia upinzani wa kisiasa.

Kadiri ya asilimia 44 ya watu wa magerezani walikuwa wale mahabusu au waliotiwa rumande. Waliotiwa ndani kwa makosa ya jinai kwa kawaida walisubiri miaka kadhaa kabla ya mashitaka yao kusikilizwa, kwa sababu ya muda unaotakiwa wa kukamilisha uchunguzi wa polisi, kukosekana kwa mahakimu wa kusikiliza kesi na pia ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kesi. Uombaji wa rushwa wa polisi na maofisa wa mahakama ulichelewesha zaidi usikilizaji wa mashitaka kwa wale ambao hawakuwa na uwezo wa

kulipa. Muda wa kuwekwa ndani kabla ya mashitaka wakati mwingine ulikuwa mrefu zaidi kuliko muda wa adhabu uliotolewa kwa watu waliotiwa hatiani katika hukumu ya uhalifu waliofanya. Wachunguzi wa mambo walikadiria kwamba takriban asilimia 5 ya watu waliowekwa rumande mwishowe walipatikana na hatia na mara nyingi wale waliopatikana na hatia walikuwa wamekwisha kutumikia adhabu yao kabla hata mashitaka yao hayajasikilizwa. Ofisa mmoja wa serikali alikisia kwamba inachukua hadi miaka mitano kwa kesi za mauaji kufika Mahakama Kuu. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka baadhi ya watuhumiwa walikuwa wametimiza miaka mingi kiasi cha 10 gerezani bila kesi zao kusikilizwa mahakamani. Mwezi Julai, Waziri wa Sheria na Katiba alitoa mwongozo akitaka mahakama za sheria kumaliza kesi zote za jinai na za madai zilizopo ndani ya siku 60 ili kupunguza idadi ya kesi zinazosubiri uamuzi mahakamani. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka hapakuwa na ripoti yoyote kuhusu maendeleo ya kufikia lengo hili.

**Msamaha**

Mwezi Februari Rais wa Zanzibar aliwasamehe watu watatu waliokuwa wametiwa hatiani kwa kuchoma moto hoteli mali ya bibi mmoja mfanyabiashara aliyekuwa mgombea wa urais wa Zanzibar wa Upinzani.

**e. Kunyimwa haki ya Kusikiliza Mashitaka kwa umma**

Katiba inatoa idara huru ya mahakama. Hata hivyo idara ya mahakama iliendelea kutopewa fedha za kutosha, fisadi, isiyo na ufanisi na yenye kuathirika na watawala. Ufisadi ulienea hasa miongoni mwa maofisa wa chini wa mahakama na makarani wa mahakama.

Wachunguzi wa kujitegemea walitilia shaka uwezo wa mfumo wa mahakama kumpa mshitakiwa hukumu ya haki na ya haraka. Makarani wa mahakama walichukua rushwa na kuamua kesi ifunguliwe na kuficha au kupotosha welekeo wa majalada ya kesi ya wale walioshitakiwa kwa uhalifu. Mara chache Mahakimu wa Mahakama za ngazi ya chini walipokea rushwa kuamua kama kuna kosa au hakuna, kutoa hukumu au kuamua kutoa rufaa za kesi kutoka mahakama za Mwanzo au za Wilaya.

Idara ya Sheria ilikabiliwa na upungufu mkubwa wa majengo ya mahakama. Mwezi Julai Wizara ya Sheria na Katiba ilinunua majengo ya mahakama kwa ajili ya ofisi za Kanda ya Mtwara na Songea na Ofisi mpya zilifunguliwa Iringa na Sumbawanga. Hata hivyo pamoja na juhudi hizi, mahakama chache tu zilipatikana kwa wananchi, na gharama za kusafiri kwenda kwenye mahakama ya karibu zilikuwa kubwa sana.

Serikali iliendelea na programu yake ya kubadili mfumo wa mahakama. Kutokana na ubia wa kuhusisha pande mbili au pande

nyingi na wahisani, katika kipindi cha mwaka huu serikali iliongeza matumizi kwa ajili ya mahakama kwa takriban asilimia 40 kwa huduma kwa ajili ya kuboresha huduma kwa waliowekwa ndani ya maeneo ya vijijini; na kwa ajili ya utawala bora kwa jumla na uendeshaji wa mahakama. Katika mwaka 2005 serikali iliongeza mara dufu fungu la gharama ililokuwa imetoa ili kukabiliana na upungufu wa ufanisi wa mahakama, ufisadi na kuboresha sifa za watumishi wake.

Msingi wa Mfumo wa Sheria ni Sheria za kawaida za Uingereza na unatambua sheria za Jadi na sheria za Kiislamu katika kesi za madai. Katika masuala ya jinai Wakristo na Waislamu hutawaliwa na sheria ya Nchi au Sheria za kawaida.

Tume ya Huduma ya Sheria chini ya uenyekiti wa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufaa, iliteua majaji wote isipokuwa wale wa Mahakama ya Rufaa na wa Mahakama Kuu ambao waliteuliwa na Rais, Mahakama zote, pamoja na Mahakama za Kiislamu za Zanzibar, zilijazwa na watumishi wa serikali.

Nchi ina mfumo wa ngazi tano wa mahakama ambao Mahakama ya Rufaa ndiyo ngazi ya juu kabisa. Zaidi ya haya, Visiwani Zanzibar ambako asilimia 95 ya watu ni Waislamu, upo mfumo wa Mahakama za Kadhi wenye mpangilio wake ambao kilele chake ni Mahakama ya Rufaa ya Kadhi. Mahakama hizi husikiliza masuala yanayohusu Sheria ya Jadi ya Kiislamu kwenye masuala ya familia na mambo yanayohusiana na hayo. Bara, Sheria ya haki za raia karibu hutawala watu wote wanaohusika katika kesi ya hifadhi ya watoto na talaka. Sheria ya Kiislamu na ya Jadi inatawala mambo mengine ya kifamilia kwa Waislamu na Wakristo kwa mpangilio huo. Huko Bara watu wote, wakiwa ni pamoja na Waislamu wako chini ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ambayo ni mkusanyiko wa sheria ya familia inayotambua ndoa za Kiislamu na za Jadi lakini huziweka chini ya utaratibu wa serikali na ulinzi wa sheria ya haki za binadamu kwa ajili ya wanawake.

Ingawa wengi wa Majaji wa Zanzibar walikuwa Waislamu, walikuwapo pia Majaji Wakristo na baadhi ya vikundi vya Kiislamu vilinung'unika ya kwamba haikuwa sahihi kwa majaji Wakristo kusimamia sheria ya Kiislamu katika masuala ya kifamilia bila kupata mafunzo ya Sheria ya Kiislamu. Viongozi wa BAKWATA, ambalo ndilo Baraza linalosimamia masuala ya Kiislamu Bara, waliomba kuanzishwe Mahakama ya Kadhi kwa ajili ya Bara. Mjadala mkali ulizuka baina ya viongozi wa Kiislamu na maaskofu wa Kikatoliki. Maaskofu walimtahadharisha Rais dhidi ya uanzishaji wa mahakama hiyo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka mabishano yaliendelea kuhusu suala hili.

Katika masuala ya kifamilia maudhui na matumizi ya baadhi ya sheria za jadi na Sheria ya Kiislamu viliwabagua wanawake, Bara na pia Visiwani Zanzibar.

Kulikuwa na Mahakama ya Watoto moja. Hata hivyo ilielemewa sana na hivyo ilishughulikia kesi za watoto wahalifu wa Dar es Salaam tu, ambapo ndipo ilipojengwa. Watoto wahalifu wa mikoa mingine walishitakiwa katika mahakama za wakubwa.

Sheria vilevile inatoa nafasi kwa Mahakama ya Biashara, Mahakama ya Ardhi, Mabaraza ya nyumba na Mahakama za Kijeshi. Mahakama za kijeshi hazisikilizi kesi za raia. Washitakiwa wa Mahakama ya kijeshi wanaweza kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

**Taarifa za Usikilizaji Mashtaka**

Mashtaka ya makosa ya jinai kwa kawaida yaliendeshwa wazi kwa umma na kwa vyombo ya habari. Hata hivyo haikuwa hivyo kwa baadhi ya mashtaka. Mahakama zilizoendeshwa mashtaka kwa siri... kama vile katika kesi za usafirishaji wa dawa za kulevya – zilitakiwa, kwa kawaida kutoa sababu za kufanya hivyo. Katika kesi zinazowahusu watuhumiwa wa kigaidi, sheria inasema ya kwamba kila mtu isipokuwa wale wanaohusika wanaweza wakaondolewa na maelezo yanaweza yakafichwa kwa madhumuni ya kulinda mashahidi wasijulikane.

Katika nchi nzima hakuna mashtaka yanayoendeshwa na hakimu na wazee wa mahakama peke yake. Washitakiwa au mawakili wao wanapata ushahidi wa serikali, wana haki ya kuhoji mashahidi na wana haki ya kuwasilisha ushahidi kwa niaba ya mshitakiwa. Washitakiwa wote wanaoshitakiwa kwa makosa ya jinai au madai...isipokuwa wale wanaofikishwa katika mfumo wa Mahakama ya Kadhi ya Zanzibar na kesi zinazohusu hali ya Sheria za Katiba ya Zanzibar... wanaweza kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa Tanzania kwa maamuzi yaliyotolewa. Sheria inatoa haki ya ushauri kwa mshatakiwa kwa washitakiwa waliofikishwa mahakamani kwa makosa ya mauaji au uhaini, na pia kwa washitakiwa masikini katika kesi kubwa nyinginezo. Kulikuwa na wanasheria waendesha mashtaka wapatao mia chache tu nchini ingawa idadi yao ilizidi kuongezeka. Washitakiwa maskini wengi walishitakiwa kwa makosa madogo zaidi hawakupata ushauri wa kisheria. Washtakiwa wengi katika sehemu za vijijini ambao hawakuweza kukodi wakili au mwanasheria, walijiwakilisha wenyewe mahakamani lakini wanawake na wahitaji wakiruhusiwa kupata msaada wa kisheria. Serikali iliamua kutoa uwakilishi wa kisheria kwa vikundi vidogo visivyo na uwakilishi wa kisheria kwa kuwataka wanasheria kushughulikia idadi maalumu ya kesi za kutolea msaada wa kisheria kwa kuzingatia mtawanyo mpana wa kijiografia. Sheria inazuia mawakili kujitokeza au kuwatetea wateja katika mahakama za kiwango cha Mwanzo.

**Wafungwa wa Kisiasa na Waliotiwa Kizuizini**

Hapakuwa na ripoti ya kuwepo wafungwa wa kisiasa au waliotiwa kizuizini.

**Taratibu za Mahakama ya Madai na Urekebishaji**
Upo mfumo huru na usio na upendeleo wa mahakama katika masuala ya madai. Taratibu za madai zinaendeshwa katika Mahakama Kuu au katika viwango vya Mahakama ya Hakimu Mkazi au Wilaya. Watu wanaweza kuleta kesi za mahakamani zinazodai uharibifu au kusimamishwa kwa ukiukaji wa haki za binadamu. Hata hivyo taratibu za mahakama za madai mara nyingi zilikwenda polepole sana, hazikuwa na ufanisi na zilikuwa na ufisadi.

**f. Udukizaji holela katika Faragha, Familia, Kaya au Mawasiliano**

Kwa jumla Sheria inazuia vitendo kama hivi kufanyika pasipo kibali cha upekuzi. Hata hivyo serikali haikuheshimu kila mara vizuizi hivi katika hali halisi. Ni mahakama tu ndizo zinazoweza kutoa vibali kama hivyo. Lakini, hata hivyo sheria inaruhusu pia upekuzi wa watu na mazingira pasipo kibali inapobidi ili kuzuia upoteaji au uharibifu wa ushahidi unaoambatana na kosa, au kama hali ni mbaya na ya haraka. Katika hali halisi watu wa vikosi vya usalama mara chache sana hutafuta kupata vibali na mara nyingi walipekua kaya binafsi na shughuli za biashara walivyotaka. Sheria inayohusiana na ugaidi inaruhusu askari polisi wa cheo fulani kufanya upekuzi bila kibali katika matukio fulani ya haraka. Hapakuwa na ripoti kwamba sheria hiyo imekwisha kutekelezwa kwa vitendo.

Tofauti na mwaka 2005, hapakuwa na ripoti kwamba vikundi vya Wanamgambo vya Zanzibar walijihusisha katika uporaji katika majumba, maduka na asasi za dini.

Inasemekana askari wa usalama walifuatilia simu na mawasiliano ya baadhi ya wananchi na wakazi wa kigeni.

Katika kipindi cha mwaka huu serikali iliwaondoa kwa nguvu au kuwahamisha watu binafsi na kubomoa au serikali kutumia tena makazi yao katika jitihada za kusafirisha maeneo ya mijini kama vile Dar es salaam na Arusha. Mwishoni mwa mwezi Septemba na mwanzoni mwa Oktoba, viongozi walifanya jitihada kwa kiwango kikubwa kuwahamisha wanunuzi na wachuuzi wadogowadogo (yaani wamachinga) walioko pote katika miji hii na kuwapeleka katika sehemu zilizotengwa kwa ajili ya shughuli hizo. Serikali iliwapa wamachinga ilani kadhaa za makusudio yake na hivyo kuhalalisha jitihada kama njia ya "kuhakikisha kwamba miji ya nchi yetu inavutia wawekezaji na kufuatilia mbali maficho ya majambazi."

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka kesi iliyowahusisha wanakijiji 135 waliodai kuwa walikuwa wamefukuzwa kinyume cha sheria kutoka katika ardhi yao na makazi yao na maofisa wa ngazi ya wilaya mnamo mwaka 2001, ilikuwa haijasikilizwa. Kesi hii iliandikishwa mwezi Juni mwaka 2005 baada ya serikali kushindwa kujibu azimio la Tume ya Haki za Binadamu na utawala

Bora ambalo liliipa serikali siku 30 kutoa fidia na kuwapa makazi wanakijiji hao na azimio hilo liliomba kwamba ripoti itolewe kuhusu jambo hili kufikia Mwezi Mei 2005.

Mpaka mwezi Machi, Visiwani Zanzibar wanawake waliopata mimba nje ya ndoa waliweza kufungwa hadi miaka miwili. Katika nadharia sheria hii iliweza kutumika kwa wanaume pia. Hata hivyo kwa kuwa upimaji wa DNA ulikuwa haupatikani Zanzibar, ni wanawake tu wameadhibiwa kwa mujibu wa sheria hii. Katika kipindi cha mwaka huu, mwanamke mmoja alitiwa hatiani kwa sheria hii na kutumikia adhabu ya kifungo cha nje. Tarehe 5 Machi, Rais Karume alitia saini Sheria inayokuwa badala ya adhabu za kifungo kwa kufanya kazi za huduma katika jamii kwa wanawake wanaopatikana na hatia katika kosa hili. Katika kipindi cha mwaka huu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Zanzibar ilichapisha kanuni zinazotaja aina ya huduma za jamii zinazoweza kuwekwa.

**Sehemu ya 2: Heshima ya Uhuru wa Raia, Vikiwemo**

**a. Uhuru wa Kuzungumza na Vyombo vya Habari**

Katiba inaruhusu uhuru wa kuzungumza lakini haitamki kinagaubaga uhuru wa vyombo vya habari. Katika hali halisi serikali ya Muungano wa Tanzania ilipunguza kwa kiasi fulani haki hizi, na serikali ya Zanzibar yenye mamlaka nusu iliweka mpaka kwa kiasi kikubwa kuhusu haki hizi. Sheria zinazopunguza uwezo wa vyombo vya habari kufanya kazi kikamilifu na mfumo ufanisi wa mahakama vilipunguza uhuru wa kuzungumza na vyombo vya habari, hasa Zanzibar ambayo ina sera tofauti na ile ya Bara.

Vyombo vya habari vya maandishi vilipaswa kutii kwa kiasi cha kutosha mipaka vilivyowekewa na serikali, ikiwa ni pamoja na uhimizaji wa kanuni ya maadili. Ingawa kanuni hii inaelezwa kuwa ni ya hiari, serikali imepiga faini na kusitisha magazeti kwa mujibu wa kanuni hii. Waandishi wa magazeti, kwa kitisho cha sheria za kukashifu watu ambazo zinatoa adhabu za makosa ya jinai, walijitahidi kujitathmini. Hata hivyo serikali ya Bara iliruhusu wapinzani wa kisiasa kuvifikia vyombo vya habari bila mpaka. Ingawaje kimsingi vyombo vya habari vinadhibitiwa na serikali huko Zanzibar, wapinzani wa serikali waliweza kuvifikia huko pia.

Chini ya utawala wa Rais Kikwete, uhuru wa kuzungumza uliongezeka. Kwa kutiwa moyo na msimamo wa Rais hadharani kuhusu uhuru wa vyombo vya habari, vyombo vya habari viliweza kuwafichua maofisa fisadi waziwazi zaidi. Kwa mfano, Mwezi Machi gazeti moja binafsi liliandika kuhusu ofisa wa ngazi ya juu wa kibalozi aliyekuwa Italia akishutumiwa na viongozi kwa kufuja $ milioni tatu (shilingi bilioni 3.8).

Vyama vya siasa vinatakiwa na sheria kuunga mkono kuendelea kuwapo kwa Muungano wa Tanzania na watu wanaotumia lugha "chafu" kuhusu uongozi wa nchi wanaweza kukamatwa. Hata hivyo vifungu hivi havikutumika katika kipindi cha mwaka huu. kwa upande wa Bara wanachama wa vyama vya upinzani na wengineo walikosoa waziwazi serikali na chama tawala. Visiwani Zanzibar mara kwa mara upinzani ulitumia mlango wa uhuru wa huko Bara kukosoa serikali ya Zanzibar. Tofauti na mwaka 2005, hapakuwa na ripoti za vizuizi kuhusu uhuru wa kuzungumza siasa na dini kwa Waislamu.

Usajili wa magazeti uliendelea kuwa mgumu na ulitegemea utashi wa msajili. Katika kipindi cha mwaka huu idadi ya magazeti, vituo vya redio na waandishi wa habari viliongezeka. Katika Bara kulikuwa na machapisho zaidi ya 785, ikiwa ni pamoja na magazeti, machapisho ya ndani ya asasi zenyewe na majarida pamoja na magazeti 14 ya kila siku na zaidi ya 20 ya kila wiki. Mengi ya magazeti ya Bara yalikuwa ya binafsi. Kulikuwa na majarida dazani moja nchini, baadhi yake yalikuwa yakimilikiwa au yaliathiriwa na vyama vya siasa yakiwamo yale ya CCM tu bali pia na yale ya vyama vya upinzani vya Civic United Front (CUF) na CHADEMA. Machapisho ya Bara, pamoja na gazeti moja linalomilikiwa na serikali, yaliikosoa serikali mara kwa mara.

Takriban vituo 33 vya redio na tisa vya televisheni pamoja na mitandao 16 ya kebo, hutangaza Dar es Salaam na maeneo machache Bara. Vituo vingi vya redio na vyote vya televisheni, isipokuwa kimoja, vilimilikiwa binafsi. Kulikuwa na vizuizi fulani vya serikali. Kwa mfano, vituo vya redio havikuweza kutangaza katika lugha za kikabila.

Kulingana na idara ya maelezo Zanzibar, wakala wa serikali, mojawapo ya magazeti mawili ya Zanzibar lilimilikiwa binafsi, na moja lilimilikiwa na serikali. Serikali ilidhibiti maudhui ya matangazo ya redio na televisheni pamoja na njia zingine zilizomilikiwa binafsi. Kisiwani Zanzibar kulikuwa na kituo kimoja cha redio kilichomilikiwa na serikali na vinne vilivyomilikiwa binafsi. Kisiwani Pemba kulikuwa na vituo viwili vya redio; kimojawapo kilikuwa tawi la kituo cha redio cha serikali kisiwani Zanzibar na kingine kilimilikiwa binafsi. Wakazi wengi wa Zanzibar waliweza kupokea zile habari zilizokuwa na vizuizi vichache zaidi kutoka Bara.

Tofauti na mwaka 2005 hapakuwa na ripoti kwamba maofisa wa serikali Bara waliwapiga waandishi wa habari. Uchunguzi ulikuwa ukiendelea kuhusu madai ya mwezi Septemba 2005 ya waandishi wa habari kupigwa na maofisa wa askari wa magereza na wengineo kwa mpiga picha Mpoki Bukuku na mhamasishaji wa haki za binadamu na ripota Christopher Kidanka ambaye alijaribu kufuatilia ufukuzwaji wa familia kadhaa kutoka katika majumba yaliyomiliki wateja na idara ya magereza. Hadi

kufikia mwishoni mwa mwaka kesi hii ilikuwa bado ikisubiri uamuzi. Waandishi wote wawili pia walikuwa wakiishitaki idara ya magereza kwa uharibifu.

Tarehe 21 Mwezi Agosti, Maripota Pasi Mipaka waliikosoa serikali kwa kutishia kumfukuzia mwandishi Kenya ambaye alionekana katika filamu ya *Darwin's Nightmare.* Maofisa walisema kwamba filamu hiyo ambayo inaelezea maliasili na ufukara katika eneo la Ziwa Viktoria iliharibu biashara na taswira ya nchi. Mkurugenzi wa filamu hiyo aliishutumu serikali kwa kuendesha "Kampeni ya vitisho" dhidi ya watu walioonekana katika filamu yake, ikiwa ni pamoja na Richard Mgamba, mwandishi mpelelezi wa gazeti la *The Citizen*. Mgamba alitoroka Mwanza tarehe 4 Agosti, maandamano kupinga filamu hiyo yalipoandaliwa na viongozi wa pale pamoja na Polisi. Viongozi wa pale walimtisha Raphael Tukiko, mlinzi wa usiku aliyeonekana katika filamu hiyo kwa kumkamata na kuamriwa kwenda kuripoti Polisi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka hapakuwa na habari zaidi kuhusu kesi hizi.

Kulikuwa na angalau ripoti moja ya kuwa watendaji wasio wa serikali waliwabughudhi au kutumia nguvu dhidi ya waandishi wa habari katika kipindi cha mwaka huu. Mwezi Aprili watu walitoa vitisho vya kifo kwa wahariri na waandishi wa habari wa gazeti la *This Day*, wakiwaonya kuhusu kutoa taarifa za rushwa katika asasi za umma. Mhariri wa gazeti hilo aliuambia mkutano wa vyombo vya habari ya kwamba mtu fulani aliwapa waandishi wa habari takriban $20,000 (shilingi milioni 25.5) kuacha kuchapisha habari za uchunguzi kuhusu maradhi ya jamii.

Mamlaka ilifuta mashitaka mawili kati ya matatu katika kesi za uchaguzi wa mwaka 2005 za wafuasi wa Chama cha CUF walioshitakiwa kwa kuwashambulia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mnamo mwezi Novemba mwaka 2005. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka Mshtakiwa wa tatu aliachiwa kwa dhamana akisubiri kesi. Visiwani Zanzibar viongozi waliendelea kuweka vizuri kwenye shughuli za maripota. Mwezi Agosti serikali ilikataa kutoa ruhusa kwa kikundi cha nje cha watangazaji wa redio cha Idhaa ya BBC kurusha matangazo kutoka Zanzibar wakati wa kipindi cha kutana - na- wasikilizaji wa Kanda. Idhaa ya BBC ilikuwa imerusha vipindi kama hivyo huko bara na katika nchi za jirani. Tarehe 10 Septemba, viongozi waliwakamata waandishi wa habari kisiwani Pemba walipokuwa wakitoka katika kijiji walimokuwa wamefanya uchunguzi kuhusu upungufu wa chakula.

Tarehe 26 Juni, huko Bara Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta jenerali, alikutana na wahariri wa vyombo vya habari vya mashirika mbalimbali binafsi kujadili njia ya kuweka mazingira ya ushirikiano baina ya polisi na vyombo vya habari. Alikiri kuwa uhusiano huo ulikuwa umejawa na uhasama, kutoaminiana na machafuko Mkuu mpya wa Jeshi la polisi alisema kwamba sasa

alitaka kuona kwamba Jeshi la Polisi na vyombo vya habari wanafikia maelewano na angependa kuendelea kuonana na vyombo vya habari kwa utaratibu wa mara kwa mara.

Makundi ya vyombo vya habari Visiwani Zanzibar yaliendelea kudai kutokomezwa kwa zile walizoziita sheria kali zisizo za lazima zinazopunguza uhuru wa vyombo vya habari. Zaidi ya hayo, waliikosoa serikali kwa kutokuwapo kwa ulinzi wa kisheria kwa vyanzo vya habari vya waandishi wa habari na wale wanaowadokezea habari.

Katika Bara waandishi wa habari na AZISE wanaoshiriki katika Mradi wa Kubadili Sheria ya Vyombo vya Habari waliendelea kuinung'unikia serikali kwamba inadhoofisha makusudi uhuru wa vyombo vya habari na kuzuia taarifa kwa vyombo vya habari kwa kutumia sheria ya mwaka 1976 inayompa Waziri wa Habari hiari kubwa ya kusitisha au kufunga kabisa magazeti na pia sheria nyingine zilizotungwa. Vilevile walikosoa sheria zinazowazuia waandishi wa habari wasiandike kuhusu magereza au polisi bila kwanza kupata kibali kutoka katika asasi hizo.

Tofauti na mwaka 2005 katika kipindi cha mwaka huu hapakuwa na ripoti za viongozi kusitisha magazeti ama Visiwani Zanzibar au Bara. Yale magazeti mawili yaliyositishwa kwa kipindi kifupi mwaka 2005, yalikuwa yakichapishwa na kusambazwa kikamilifu katika kipindi cha mwaka huu.

Kulikuwa na taarifa za ubaguzi uliofanywa na serikali kuhusu bei za karatasi za kuchapia magazeti. Hata hivyo, tofauti na mwaka 2005, hapakuwa na taarifa zilizohusu kwamba serikali ilitoa matangazo yake kwa uangalifu katika magazeti binafsi yaliyopendelewa.

Mwezi Agosti Wabunge kadhaa waliwanung'unikia wamiliki wa vyombo vya habari kwamba wamiliki hao walitumia vyombo hivyo kutangaza maslahi yao binafsi, jambo ambalo walisema ulikuwa ni utumiaji mbaya wa umiliki. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Bwana Muhammed Seif Khatibu alisema kwamba hali hiyo ilikiuka sera ya Habari na utangazaji ya nchi inayovitaka vyombo vya habari vitumike kwa manufaa ya umma. Lakini kinyume cha hili, Visiwani Zanzibar ofisa mmoja katika Wizara ya Habari, alisema mwezi Agosti kwamba nia ya vyombo vya habari ilikuwa ni kutunza amani, kwa maana kwamba taarifa zenye ukinzani hazikuwa na nafasi.

Kitisho cha kutumia sheria kuhusu kashfa, ambayo hutoa adhabu kwa makosa ya jinai, kiliwaogofya waandishi wa habari na kusababisha waandishi wa habari wengi kuzingatia tathmini binafsi. Ingawa sheria inataja wazi mshitaki anapaswa kuthibitisha nia ya ovu, wachunguzi wengi wa vyombo vya habari waliikosoa mahakama kwa kudharau kifungu hiki na kutoa kwa

vyombo vya habari adhabu kali, na nzito zilizokuwa zimechochewa kisiasa. Hata hivyo hapakuwa na taarifa ya matukio maalumu ya vitendo hivyo katika kipindi cha mwaka huu kwa mujibu wa Baraza la Vyombo vya Habari, Asasi za mafunzo na waandishi wa habari.

Serikali ya Zanzibar ilitaja usalama wa umma kama kisingizio cha kuficha maoni ambayo iliyaona hayakubaliki kisiasa. Baada ya kulifunga gazeti binafsi la Dira mwaka 2004, viongozi wa Zanzibar waliendelea kuwabughudhi wahariri wake. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka huu serikali ilitoa pasipoti kwa Nabwa (tazama sehemu ya 2.d).

Ukosekanaji wa kupata taarifa za serikali wa vyombo vya habari, uliendelea kuwa tatizo kubwa. Katika hotuba yake katika kipindi cha mwaka huu, Rais alihimiza watumishi wa serikali kutoa habari kwa vyombo vya habari wanapotakiwa kufanya hivyo na baadhi ya asasi za serikali zilianza kufanya hivyo. Hata hivyo, Rais hakusema kwamba kanuni za utumishi wa umma zinazuia wafanyakazi wa serikali wasitoe habari za serikali kwenye vyombo vya serikali. Kizuizi hiki kinaruhusu wawakilishi wachache tu wa ngazi za juu wa serikali kutoa habari kwenye vyombo vya habari (tazama sehemu ya 3).

Mwezi Mei chama cha watu binafsi wenye kuvutiwa katika vyombo vya habari, --- wanataaluma, maofisa katika Wizara ya Habari, wamiliki wa vyombo vya habari binafsi na wawakilishi wa umoja wa raia--- kilihimiza serikali kubadilisha sera ya vyombo vya habari ya mwaka 1994 ili kuvipa vyombo vya habari msukumo huru zaidi wa kuupa umma habari na kupiga marufuku vizuizi vinavyozuia kituo chochote cha redio binafsi au televisheni binafsi kutangaza kwa eneo zaidi ya asilimia 25 ya taifa. Hakuna hatua iliyokuwa imechukuliwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Vyombo vya habari ya Kusini mwa Afrika, uhuru wa vyombo vya habari uliendelea kutishiwa kutokana na kukosa mafunzo, mishahara midogo na ufisadi katika taaluma ya uandishi wa habari.

**Uhuru wa Intaneti**

Hapakuwa na vizuizi vya serikali kuhusu upatikanaji wa Intaneti au ripoti kwamba serikali ilifuatilia baruapepe au maeneo chati. Watu binafsi na vikundi waliweza kushiriki katika utoaji wa amani wa maoni kupitia katika intaneti ikiwa ni pamoja na kupitia baruapepe. Idadi ya vibanda vya intaneti na watoaji wa intaneti iliongezeka katika kipindi cha mwaka huu. hata hivyo ni asilimia 10 tu ya wananchi ilikuwa na upatikanaji wa umeme na hivyo kuwa kipingamizi kikubwa sana cha upatikanaji wa huduma hizi kwa jumla.

**Uhuru wa Taaluma na Matukio ya Utamaduni**

Hapakuwa na vizuizi vya serikali kuhusu uhuru wa taaluma au matukio ya utamaduni

**b. Uhuru wa Mkusanyiko wa Amani na Ushirikiano**

**Uhuru wa Mkusanyiko**

Katiba inaruhusu kuwepo uhuru wa mkusanyiko, na kwa jumla serikali iliheshimu haki hizi kwa vitendo katika kipindi cha mwaka huu.

Serikali inawataka watayarishaji wa mikutano kupata kibali cha polisi kabla. Polisi wana uwezo wa kukataa kutoa kibali kwa sababu ya usalama wa umma au kwa misingi ya usalama au iwapo anayetafuta kibali hicho ni mwanachama wa shirika au chama ambacho hakijasajiliwa. Katika kipindi cha mwaka huu, mamlaka ziliwakamata wananchi kwa kukusanyika bila kibali kinachohusika. Kwa mfano kwa mujibu wa gazeti la *Msemakweli* la tarehe 25 Juni, askari polisi Mkoani Rukwa waliwatawanya kwa nguvu wahubiri kutoka mikoa mbalimbali kwa kukutana na kuhubiri bila kibali.

Hapakuwa na ripoti ya kwamba serikali ililizuia vyama vya upinzani kufanya mikutano huko Bara katika kipindi cha mwaka huu. Hata hivyo mwezi Mei viongozi Visiwani Zanzibar walikinyima Chama cha CUF kibali cha kufanya maandamano na kutembea ili kupinga matakwa ya Spika kwamba apatie maswali ya upande wa Upinzani kabla hawajayawasilisha katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Viongozi hawakutoa kibali lakini waliruhusu maandamano ya hadhara.

Tofauti na mwaka 2005, wakati askari wa usalama walipoingilia mara kadhaa uhuru wa wananchi kukusanyika kwa amani, hasa kwa sababu za kisiasa au maandamano, hapakuwa na ripoti ya kuingilia kwa aina hiyo katika kipindi cha mwaka huu.

Mwezi Oktoba serikali iliondoa amri ya kupiga marufuku maandamano ya Uamsho (ambao pia unajulikana kama Uhuishaji wa Kiislamu au Kituo cha Uenezaji wa Kiislamu), ambalo ni shirika la ufadhili wa vyama ambavyo havina dhima vya Kiislamu. Uamsho kiliomba ulinzi wa polisi wakati wa maandamano ya kupinga matukio ya nchini Iraq na serikali ikaridhia ombi hilo (tazama sehemu ya 2.C).

**Uhuru wa Ushirikiano**

Katiba inaruhusu kuwepo kwa uhuru wa kushirikiana na kwa jumla serikali iliheshimu haki hii kwa vitendo, ingawa serikali iliendelea kuweka masharti katika kusajili vyama vya siasa. Vyama visivyosajiliwa vilizuiwa kusimamisha wagombea katika

uchaguzi wa mwaka 2005 lakini kutokuwepo kwa uchaguzi katika kipindi cha mwaka huu, kizuizi hiki hakikutumika.

Msajili wa vyama vya siasa ana mamlaka kamili ya kuthibitisha au kukataa usajili wa chama chochote cha siasa na ana jukumu la kutekeleza kanuni kwenye vyama vilivyosajiliwa. Kwa mujibu wa sheria, wananchi hawawezi kuunda vyama vipya vya siasa kiholela tu bali sharti watii masharti fulani kuvisajili katika ofisi ya msajili.

Vyama vilivyopata usajili wa muda vinaweza kufanya mikutano ya hadhara na kuandikisha wanachama. Ili kupata usajili wa kudumu na kuwa na haki ya kusimamisha wagombea kwa ajili ya uchaguzi, vyama vyenye usajili wa muda hupewa miezi sita kuwasilisha orodha ya wanachama wasiopungua 200 katika mikoa 10 kati ya mikoa 26 ya nchi, ikiwa ni pamoja na mikoa miwili kati ya mikoa mitano ya Zanzibar.

Katika kipindi cha mwaka huu serikali iliendelea kutekeleza masharti ya kisheria ya kwamba AZISE zijisajili kwenye kitengo cha uratibu kilichoteuliwa na serikali (tazama sehemu ya 4). Kushindwa kujisajili au kutotimiza masharti yoyote mengine ya sheria ni kosa la jinai.

Mnamo mwezi Mei, viongozi wa serikali ya Muungano na maofisa wa serikali ya Zanzibar walikubaliana kwamba tume ya serikali kwa kiasi fulani inayoshughulika na haki za binadamu iliyokuwa ikifanya kazi Bara ingeruhusiwa kufanya kazi Zanzibar pia kufuatia marekebisho katika Sheria ya Bara ya haki na binadamu na utawala bora. Pande hizi zilikubaliana kwamba Waziri wa Zanzibar mwenye dhamana ya Utawala bora angeruhusiwa kuwasilisha matokeo yoyote ya ukiukaji wa haki za binadamu visiwani Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuliko katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, na kwamba Waziri mwenye dhamana ya haki za binadamu na utawala bora wa Bara angekutana na Waziri mwenziye wa Zanzibar kabla ya kuweka kanuni yoyote ambayo ingeiathiri Zanzibar.

**c. Uhuru wa Dini**

Katiba inatoa uhuru wa dini. Hata hivyo kulikuwa na mipaka fulani kuhusu uhuru wa dini.

Serikali inavitaka vikundi vya dini kujiandikisha kwa Msajili katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Kusajili kikundi cha dini kinapaswa kuwa na angalau wafuasi 10 na kinapaswa kuwasilisha katiba, tawasifu za viongozi wake na barua ya mapendekezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya pale patakapokuwa maskani ya kikundi hicho. Vikundi vya Kiislamu Bara pia vilitakiwa kuwasilisha barua kutoka BAKWATA, baraza linalotawala mambo ya Kiislamu Bara na kwa Zanzibar, barua ya Mufti. Vyombo hivi hupendekeza kuthibitishwa au kukataliwa kusajiliwa kwa Msajili

Mkuu wa Serikali. Katika kipindi cha mwaka huu hapakuwa na ripoti kwamba serikali ilikataa kusajili kikundi chochote Bara. Hata hivyo Visiwani Zanzibar Mufti alipendekeza kutosajiliwa kwa vikundi viwili, kikundi kimoja cha Ahmadia na kikundi kingine cha Bahai kwa sababu ya ukinzani unaodaiwa upo baina ya imani zao na imani ya Kiislamu. Kikundi cha Ahmadina kilifungua mashitaka dhidi ya ofisi ya Mufti kutokana na pendekezo hilo na hadi kufikia mwishoni mwa mwaka kesi ilikuwa ikisubiri.

Sheria inakataza kuhubiri au kutawanya vitu vinavyochukuliwa kuwa ni vya kichochezi au vyenye tishio kwa usalama wa umma. Wakati wa kipindi cha mwaka huu serikali mara kwa mara ilikataa maombi ya vikundi vya dini vya kutaka kufanya maandamano kwa sababu ya uwezekano kwamba mkusanyiko ungeweza kuwa wenye mapambano au kuchochea migogoro ya kidini.

Tarehe 22 Agosti, Mahakama ya Wilaya ya Kigoma ilimpiga marufuku mchungaji wa Kikristu Cecil Simbulanga kutokana na "mahubiri ya kichochezi" ambayo yalitukana Uislamu; Simbulanga baadaye alitolewa kwa dhamana. Tarehe 16 Oktoba Mahakama ilimruhusu Simbulanga kuhubiri tena kwa masharti kwamba asitoe matamko dhidi ya Uislamu. Tarehe 22 Desemba Simbulanga alikamatwa tena na kufikishwa mahakamani kwa kutukana Uislamu wakati akihubiri. Alikataliwa dhamana na hadi kufikia mwishoni mwa mwaka aliendelea kuwa kizuizini.

Vyombo vya habari vilitoa taarifa mwezi Juni kwamba kikundi cha wahubiri wa dini tofauti walifukuzwa na polisi mkoani Rukwa kwa kujikusanya na kuhubiri bila kibali (tazama sehemu ya 2.a)

Hapakuwa na habari zaidi kuhusu wanawake wawili Wakristu ambao walikamatwa Jijini Dar es Salaam mwezi Agosti 2005 na kushitakiwa kwa kosa la kuchoma moto Kurani.

Mwezi Septemba Serikali ya Zanzibar ilifuta mashitaka dhidi ya viongozi wawili wa Uamsho waliokuwa wameshitakiwa mwaka 2004 kwa kosa la kufanya maandamano bila kibali.

Amri ya serikali ya kupiga marufuku, katika hali ya agizo la utawala, ikizuia vikundi vya dini kujiingiza katika siasa, iliendelea kuwa na nguvu. Zaidi ya hayo wanasiasa walizuiwa kisheria kutumia lugha iliyolenga kuchochea kikundi kimoja cha dini dhidi ya kingine, au kuhimiza vikundi vya dini kupigia kura vyama fulani vya siasa. Sheria inatoa faini na muda katika jela kwa vyama vya siasa vinavyoendesha kampeni katika nyumba za ibada au vifaa vya elimu. Hata hivyo, mwaka 2005 viongozi kadhaa wa dini walitaka kujiingiza katika siasa na mamlaka haikuweka vikwazo.

Sera ya serikali inazuia ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa msingi wa imani za kidini au vitendo vya aina hiyo. Hata hivyo, vikundi vya Kiislamu viliendelea kudai kwamba serikali iliwabagua katika ajira za serikali, elimu na utekelezaji wa sheria, wakati vikundi vya Kikristo vilinung'unika kwamba serikali iliwapa Waislamu vyeo vyote nyeti serikalini. Tarehe 27 Mwezi Juni, kutokana na uteuzi uliofanywa na Rais mpya aliyechaguliwa wa Waislamu kushika vyeo nyeti vingi serikalini, Maaskofu Wakatoliki walitoa tamko wakimhimiza kuepuka upendeleo katika uteuzi serikalini. Wawakilishi wa Waislamu waliisihi serikali kuanzishwa kwa Mahakama za Kadhi na Sharia Bara kwa ajili ya kusikiliza na kutoa hukumu za kesi za masuala ya Kiislamu. Vikundi vya Kikristu vilionya kwamba mahakama kama hizo zingekiuka sifa ya serikali ya kutopendelea upande wowote baina ya dini mbalimbali na kwamba Katiba ya Muungano haikutamka Mahakama ya Kadhi mle. Viongozi wa dini ya Kiislamu, pamoja na Mufti Mkuu wa BAKWATA, walihimiza Wakristu wasiingilie masuala yaliyowahusu Waislamu.

Mwezi Juni, Maaskofu Wakatoliki walimwomba Rais kwa niaba ya serikali aingilie katika kile walichokieleza kama ni unyimaji wa haki wa uhuru wa kuabudu katika hali ya "mihadhara iliyoenea ya kashfa za dini" ambayo ingeweza kulipua kwa urahisi migogoro ya kidini na uvunjaji wa amani. Rais alijibu kwamba kwa kuwa nchi hii haina dini, serikali isingejihusisha na upande wowote dhidi ya madai ya kashfa za kidini. Hata hivyo aliuonya umma dhidi ya matumizi mabaya ya uhuru wa kuabudu.

Visiwani Zanzibar "Sheria ya Mufti" inampa mamlaka Rais wa Zanzibar kuteua Kiongozi wa dini au Mufti wa Zanzibar ambaye hufanya kazi kama mtumishi wa serikali ya Zanzibar. Mufti anaaswa kuthibitisha usajili wa vyama vya Kiislamu na kusimamia misikiti ya Zanzibar. Baadhi ya vikundi vya Kiislamu vilidai kwamba sheria hiyo huipa serikali ya Zanzibar uwezo isivyo haki katika masuala ya dini.

**Matumizi mabaya kijamii na Ubaguzi**

Ingawa kwa jumla uhusiano kati ya dini katika jamii uliendelea kuwa wa amani, kulikuwa na mgogoro kwa namna fulani kati ya Waislamu na Wakristo na taarifa moja ya vurugu za kidini katika jamii. Kanisa moja katika Wilaya ya Temeke jijini Dar es salaam lilichomwa moto tarehe 12 Februari, siku chache baada ya wezi kuliibia kila kitu. Hapakuwa na ripoti za maendeleo ya kuwakamata watu waliochoma Kanisa la Kikatoliki katika Wilaya ya Mikese katika Mkoa wa Morogoro mnamo mwezi Aprili, 2005 au kuhusu wanaume wa Kiislamu waliompiga mchungaji na Shemasi jijini Dar es Salaam mwezi Septemba mwaka 2005. Vilevile mwezi Septemba mwaka 2005, Vijana wa Kiislamu waliingia katika shule moja ya Msingi katika wilaya ya Temeke, Jijini Dar es salama na kuwapiga

kundi la walimu wa dini kwa kuwafundisha wanafunzi wa Kiislamu kuhusu Ukristo.

Mwaka 2005 kulikuwa na ripoti kwamba baadhi ya mikutano ya dini ya Kiislamu katika vituo vya mijini, baadhi ya washiriki walidharau dini ya Kikristo ambapo tendo hilo lilisababisha kupigana.

Idadi ya Wayahudi ilikuwa ndogo sana, na hapakuwa na ripoti kuhusu vitendo dhidi ya wasemiti.

Kwa ajili ya mjadala wa kina zaidi, tazama Ripoti ya Kimataifa ya uhuru wa Dini ya Mwaka 2006 (International Religions Freedom Report, 2006).

**d. Uhuru wa Kutembea Ndani ya Nchi, Usafiri Nje ya Nchi, Uhamaji na Urejeshaji watu Makwao**

Katiba inaruhusu haki hizi na kwa jumla serikali iliziheshimu. Hata hivyo, uzembe wa umangimeza na ufisadi vilizuia utu na heshima na haki ya kwenda kuishi uhamishoni iliendelea kupata mapengo ya upungufu mara kwa mara.

Wakati mwingine Polisi katika vituo vya Ukaguzi walidai hongo.

Pasipoti kwa ajili ya safari za nje ilikuwa vigumu kuzipata wakati mwingine hasa kwa sababu ya uzembe wa kiumangimeza na kuombwa hongo na maofisa. Hata hivyo muda wa kusubiri ulikuwa siku tatu kwa wastani.

Sheria hairuhusu kulazimisha wananchi kwenda uhamishoni na katika vitendo vyake serikali haikutumia nguvu ya kulazimisha wananchi kwenda uhamishoni.

Baada ya uchaguzi wa Rais mwezi Oktoba 2005 Visiwani Zanzibar, takriban Wazanzibar 100 waliodai kuwa wanachama wa CUF walikimbilia Kenya ikisemekana kwa hofu ya kuteswa na askari waliokuwa wakiiunga mkono CCM. Chama cha CUF kilikana kwamba walikuwa wanachama wa CUF na kilionyesha kwamba hakikujua lolote kuhusu hatima ya Wazanzibari hao.

Tofauti ya miaka ya nyuma hapakuwa na mashitaka kuwa Mkurugenzi wa Uhamiaji alitumia sheria ya uraia kukataza uraia kwa sababu binafsi za upendeleo.

Mnamo Mwezi Aprili serikali ilimpa Pasipoti Ali Nabwa, Mkurugenzi Mhariri wa gazeti la zamani la Zanzibar lililoitwa *Dira.* Hata hivyo haikumrudishia uraia wake. Ali Nabwa alikuwa amenyang’anywa uraia wake mwaka 2004 kwa kuchapisha makala zilizokosoa maofisa wa serikali na pia kwa kufichua

ufisadi serikalini. Mwezi Agosti idara ya Uhamiaji ya Zanzibar ilimwarifu Nabwa kwamba kwa kuwa "hakuwa raia wa Tanzania" na alikuwa mtu asiyetakiwa Zanzibar anapaswa kulipa $ 400 (yaani shilingi 510,000) kwa ajili ya kupata kibali cha muda cha uraia au $ 600 (shilingi 765,000) kwa kibali cha kudumu. Nabwa alidharau ilani hiyo ya Zanzibar akisema kuwa ni ngazi ya Muungano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo iliyokuwa na kauli ya mwisho kuhusu uraia. Hata hivyo, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka alikuwa hajapata ilani rasmi kuhusu hali ya uraia wake.

**Ulinzi wa Wakimbizi**

Sheria inatoa nafasi ya kuridhia ukimbizi au kuwapa hifadhi wakimbizi kwa mujibu wa Makubaliano ya Baraza la Umoja wa Mataifa ya mwaka 1951 yanayohusu Hali ya Wakimbizi protokali yake ya mwaka 1967 na serikali imeweka mfumo wa kutoa ulinzi kwa wakimbizi. Hata hivyo katika hali halisi serikali haikutoa ulinzi *dhidi ya kushitakiwa* kuhusu urejeaji wa watu katika nchi ambako walihofu kushitakiwa. Serikali iliwarudisha zaidi ya Warundi 1,700 na Wanyarwanda 15,000 waliobainishwa kuwa wahamiaji waliokuwa kinyume cha sheria na hawakuwa wameshirikiana na shirika la UNHCR kuhakikisha kwamba hakuna aliyekuwa na kibali halali cha ukimbizi. Mara fulani fulani serikali pia ilishindwa kuliarifu shirika la UNHCR kuhusu kuja kwa waombaji wapya wa hifadhi na haikuruhusu UNHCR kuwapo mipakani wakati wa ukaguzi wa wakimbizi. Katika kipindi cha mwaka huu mara fulani serikali ilikataa kukubali uingiaji wa wale waliotaka hifadhi au ukimbizi mipakani na ulishindwa kuendesha kwa wakati maamuzi ya hali ya ukimbizi.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka kulikuwa na takriban wakimbizi 685,000 nchini, hasa kutoka Burundi na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) wakiwemo takriban wakimbizi 285,000 katika takriban kambi 14 zinazosaidiwa na UNHCR upande wa Kaskazini Magharibi wa nchi yetu. Karibu wakimbizi 400,000 walikuwa katika makazi au vijiji vya wakimbizi vinavyojitosheleza. Pia kulikuwa na takriban Wasomali 2,700 walioishi katika kambi ya pwani na walipokea msaada fulani wa UNHCR.

Iliendelea kuwa kinyume cha sheria kukaa nje ya kambi zao au makazi yao au kusafiri nje ya kambi zao bila vibali, ingawaje waliruhusiwa kuokota kuni ndani ya eneo la maili mbili na nusu ya kambi zao. Mara nyingi wakimbizi walisafiri zaidi ya maili tano nje ya kambi zao kuokota kuni kwa sababu hazikupatikana katika maeneo ya jirani. Wakimbizi hawa ambao kwa kawaida ni wanawake na watoto mara nyingi walikuwa waathirika wa wizi, kudhulumiwa na kubakwa. Katika kipindi cha mwaka huu matukio kama hayo yalipungua baada ya maofisa kuwahimiza wakimbizi kutembea katika vikundi, ripoti ya tukio moja tu la kubakwa ndiyo iliyotolewa kati ya mwezi Oktoba na Desemba.

Wakimbizi waliokamatwa nje ya maeneo yaliyotengwa bila vibali, hasa katika maeneo ya mijini kama vile Dar es Salaam, walikabiliwa na kukamatwa na kupata kifungo cha miezi sita au kupigwa faini ya takriban $ 39 (shilingi 50,0000). Katika kipindi cha mwaka huu takriban wakimbizi 1,000 na wahitaji wa hifadhi waliokutwa nje ya kambi bila vibali waliadhibiwa kwa kuwapo huko kinyume cha sheria. Serikali iliahirisha mkabala wake kwa makosa madogo ya wakimbizi ya kuwashitaki kwa mujibu wa sheria ya wakimbizi ambayo inataja kutiwa kizuizini hadi siku tatu au kufanya kazi za jumuiya au vyote viwili. Sheria ya Uhamiaji inataja kifungo cha miaka miwili ikifuatiwa na kurudishwa katika nchi walikokuwa wakiishi wakati wakiomba ukimbizi.

Shirika la UNHCR, kwa kushirikiana na serikali liliendelea kutoa usalama kwa wakimbizi. Hata hivyo, uhalifu---- yakiwamo mauaji, wizi, ubakaji na vurugu za ndani---- viliendelea kuwa tatizo kubwa ndani na kandokando ya kambi za wakimbizi. Katika kipindi cha mwaka huu, serikali ilipeleleza, ilishitaki na kuwaadhibu wakosaji wa kutukana matusi katika kambi za wakimbizi lakini kesi nyingi zilizohusisha uhalifu na utukanaji nje ya kambi zilipelekwa kwa mamlaka ya mtaa. Wakazi wa kambi za wakimbizi waliathirika sana kwa kucheleweshwa na uwezekano mdogo wa kupatikana kwa mahakama ambayo ni matatizo ya kawaida yanayowakabili raia pia. Kulikuwa na ripoti kwamba baadhi ya wakimbizi walijihusisha katika shughuli za usungusungu ndani ya kambi wakati mwingine wakipiga wakimbizi wengine. Tofauti na mwaka 2005, hapakuwa na ripoti kwamba polisi waliowekwa katika kambi za wakimbizi walitumia nafasi hiyo kufanya ngono na wakimbizi wa kike au kwamba wanawake na watoto walijihusisha na vitendo vya ngono ndani ya kambi.

Wakimbizi wa Burundi na Kongo waliendelea kurejea makwao wakiwa wamevutiwa na kuongezeka kwa usalama nchini Burundi na DRC na pia kutokana na uhimizwaji mkubwa kutoka serikalini na msaada wa shirika la UNHCR. Tarehe 20 mwezi Juni tume ya vyombo vitatu iliyokuwa imeundwa na shirika la UNHCR na serikali za Tanzania na Burundi ilitangaza kwamba kuanzia mwezi Septemba "ingekuza" kuliko tu "kuwezesha" urejeshaji wa hiari wa wakimbizi Burundi. Zaidi ya wakimbizi 40,000 wa Burundi walirudi nyumbani katika kipindi cha mwaka huu. Shirika la UNHCR liliendelea kuwezesha urejeshaji wa hiari wa wakimbizi kwenda DRC na zaidi ya wakimbizi 20,000 walirejea katika kipindi cha mwaka huu. Idadi kubwa ya wale waliorudi ilikuwa ya wale waliorudi kwa hiari. Hata hivyo baadhi ya wakimbizi walirudi kwa kitisho cha ulinzi dhidi ya kushitakiwa au kuwekewa vizuizi kwenye shughuli zao nchini Tanzania. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka huu, Mkuu wa Wilaya ya Kibondo aliendelea kutembelea kambi za wakimbizi na kuwahimiza

wakimbizi kurudi mwakao. Kizuizi cha wakimbizi kukaa katika kambi zao pia kilisaidia kurejesha wakimbizi makwao.

**Sehemu ya 3 Heshima kwa Haki za Kisiasa:**
**Haki ya Raia Kubadilisha Serikali Yao**

Katiba inawapa raia haki ya kubadili serikali yao kwa amani, na raia walitumia haki hii katika uchaguzi wa Zanzibar na Bara. Hata hivyo vifungu vya kisheria na kifedha vilivyokipendelea chama tawala cha CCM, ukiukaji wa taratibu za uchaguzi, na vurugu za kisiasa zilipunguza ufanisi wa utaratibu wa uchaguzi Visiwani Zanzibar.

**Ushiriki katika Uchaguzi wa Siasa**

Uchaguzi tofauti hufanywa Bara na Visiwani Zanzibar, ingawaje wakati mwingine siku ileile, ambapo raia wa pande zote mbili za Muungano huchagua maofisa wa mahali pao, Wabunge wa Bunge la Muungano na Rais wa Muungano. Zaidi ya hayo, Wazanzibari humchagua Rais wa Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika kura ambazo watu wa Bara hawashiriki.

Mwezi Desemba mwaka 2005, Jakaya Kikwete, mgombea wa CCM, alichaguliwa kuwa Rais kwa asilimia 80.2 ya kura zilizopigwa katika uchaguzi ambao watazamaji wa kimataifa walisema kuwa ulikuwa huru na wa haki zaidi kuliko uchaguzi uliotangulia. Hata hivyo, kampeni zilizokuwa zimetangulia uchaguzi huo zilikuwa na vurugu katika baadhi ya mikoa. Katika uchaguzi wa Wabunge chama cha CCM kilishinda viti 206 kati ya viti 233 vilivyopigiwa kura katika Bunge la Muungano, chama cha CUF kilishinda viti 19.

Mwezi Oktoba wapiga kura Visiwani Zanzibar vyenye uhuru kwa kiasi fulani, walimchagua Rais, Wabunge na Wawakilishi wa Visiwani. Mgombea wa CCM, Amani Karume rais aliyekuwapo, alishinda kiti cha Urais wa Zanzibar kwa asilimia 53 ya kura katika uchaguzi uliokuwa na dosari za uvunjaji wa taratibu za uchaguzi na vurugu.

Bughudha kwa vyama vya siasa zilitoweka kwa kiasi cha kutosha katika kipindi cha mwaka huu ikilinganishwa na mwaka wa uchaguzi wa 2005.

Katika Zanzibar, hasa katika Kisiwa cha Pemba, wanachama wa vyama vya upinzani walidai kwamba serikali ilikuwa ikiwabagua katika kuajiri. Serikali ndiye aliyekuwa mwajiri mkuu Visiwani Zanzibar.

Tarehe 6 Februari, Lucas Omahe Galani alihukumiwa kifungo cha miaka 10 jela kwa kosa la kumshambulia mgombea wa Urais, Jakaya Kikwete wakati wa mkutano mjini Mwanza.

Mwezi Juni Mahakama ilifuta kesi kutokana na kukosoa ushahidi dhidi ya takriban wafuasi 46 wa chama cha CUF walioshitakiwa mwaka 2005 kwa kuchochea vurugu zilizohusiana na uchaguzi katika Jimbo la Uchaguzi la Donge la Mkoa wa Zanzibar Kaskazini.

Tofauti na mwaka 2005 hapakuwa na ripoti kwamba serikali ilidhibiti wanasiasa wapinzani kwa kukataa maombi yao ya vibali vya kufanya mikutano au kwa kuwabughudhi na kuwatia ndani kwa vipindi vya muda mfupi.

Watu binafsi na vyama viliweza kutangaza kwa uhuru ugombea wao na kusimama kwa ajili ya kuchaguliwa. Hata hivyo kulikuwa na vizuizi vya Serikali kwa wagombea wanasiasa. Sheria inawazuia watu kugombea vyeo mpaka wawe wamewakilisha chama kilichosajiliwa. Inavitaka vyama vyote viliyosajiliwa kutetea Muungano na Zanzibar na inazuia vyama vyenye msingi wa kikabila, mkoa au madhehebu ya dini.

Wagombea wa CCM wamekuwa wakichaguliwa tena na tena tangu uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi. Sehemu ya nguvu yake ya kisiasa imetokana na vizuizi vya kiserikali kwenye upinzani wa kisiasa na pia kutokana na kusambaratika na ukosefu wa fedha wa vyama vingi vya upinzani. Zaidi ya hayo sheria ya uchaguzi inaagiza Wabunge wanapomaliza kipindi chao kupewa $ 15,686 (shilingi milioni 20) kama “kiinua mgongo” ambazo Wabunge waliopo hutumia kuwawezesha kuchaguliwa tena. Asasi kadhaa zisizo za Kiserikali na vyama vya upinzani vilikosoa kifungu hiki vikisema kwamba kifungu hiki kilikuwa kinafanya hali inakuwa ngumu sana kwa wale wagombea watokao katika vyama vya upinzani wanaotamani kugombea Ubunge kuweka upinzani wenye nguvu na usawa. Wafuasi wa CCM hata hivyo, walivilaumu vyama vya upinzani kwa kuwasimamisha wagombea wasiojulikana wakati wa vipindi ya uchaguzi badala ya kujenga misingi imara ndani ya umma na pia kwa kujikita katika sehemu za mijini badala ya sehemu za vijijini ambako ndiko waishiko wapiga kura wengi.

Sheria inataka kwamba wanawake wapate angalau asilimia 30 ya viti katika Bunge. Wanawake huteuliwa na vyama vyao vya siasa kuhudumia katika viti walivyotengewa, kulingana na idadi ya viti ambavyo chama chao kilishinda katika uchaguzi. Baada ya uchaguzi wa mwaka 2005 kulikuwa na viti 75 maalumu kwa wanawake. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka kulikuwa na wanawake 91 katika Bunge lenye viti 320. Wanawake walikuwa na viti 18 katika Baraza la Wawakilishi lenye viti 81 huko Zanzibar na walikuwa na vyeo vinne katika Baraza la Mawaziri la serikali ya Zanzibar. Baada ya kuingia ofisini mwezi Desemba mwaka 2005, Rais Kikwete aliteua mawaziri saba wanawake katika serikali (ikilinganisha na wanne katika utawala uliopita) na wanawake 10 Manaibu Waziri. Baadhi ya wanawake hawa waliteuliwa kuongoza idara muhimu kama vile wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Fedha na

Sheria. Katika kipindi cha mwaka huu angalau wanawake saba walifanya kazi kama majaji wa Mahakama Kuu na mwanamke mmoja alifanya kazi kama Jaji wa Mahakama ya Rufaa ya Muungano. Kulikuwa na Mawaziri 11 wenye asili ya Kiasia katika Bunge lenye viti 320.

**Ufisadi na Uwazi wa Serikali**

Mbali na uboreshaji katika muongo uliopita, ufisadi uliendelea kuwa tatizo lililosambaza kote serikalini. Kulikuwa na utambuzi mkubwa wa ufisadi, ikiwa ni pamoja na wizi, udanganyifu na shughuli za uongo za manunuzi. Ufisadi ulienea sana hasa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2005.

Kulikuwa na uwajibikaji mdogo katika vyombo vingi vya serikali. Kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2004, Wizara ya Afya haikuweza kutoa maelezo ya zaidi ya nusu ya bajeti yake ya mwaka huo.

Mnamo mwezi Aprili matokeo yaliyochapishwa na Utafiti kuhusu Upunguzaji wa Umaskini (Research on Poverty Alleviation) yalionyesha kuwa asilimia 62 ya watu waliojibu wanaona kuwa serikali ilikuwa inajitahidi vizuri katika kushughulikia ufisadi. Utambuzi wa umma kuhusu kiwango cha ufisadi miongoni mwa maofisa wa serikali ingawa kiliendelea kuwa juu, kilitamka kwa kiasi cha kuweza kuonekana. Kwa mfano, kiwango cha asilimia cha polisi kutambulika kwamba wanajihusisha katika vitendo vya ufisadi kilishuka kutoka asilimia 80 kufikia asilimia 72 na ile ya maofisa walichaguliwa kwa kura, kutoka asilimia 58 kufikia asilimia 38 kaitika miaka miwili iliyopita.

Taasisi ya Transparency International iliripoti katika Kipeuzi cha Utambuzi wa Ufisadi kwamba wananchi walitambua kwa kiwango cha chini kidogo cha ufisadi kuliko kile cha mwaka 2004 lakini waliona kwamba ufisadi ni tatizo "kubwa". Nafasi ya tathmini ya nchi haikubadilika tangu mwaka 2005.

Ripoti ya Global Integrity Report iliyotolewa katika kipindi cha mwaka huu, kutokana na utafiti wa waandishi wa habari zaidi ya 200 ilikadiria nchi hii kuwa "dhaifu sana" kwa jumla ikiwa imefanya vibaya katika maeneo yaliyosambazwa kutoka "dhidi ufisadi" mpaka "uwajibikaji wa serikali"

Kwa maelekezo ya Rais, viongozi walichukua hatua za kuboresha uwajibikaji serikalini katika kipindi cha mwaka huu. Kwa mfano, Wizara ya Ardhi na Makazi ya Watu ilifuta ushikiliaji wa ardhi wa muda mrefu (hatua ambayo inakaribia umiliki wa ardhi yote nchini ni mali ya serikali)ambayo ilikuwa haijaendelezwa kwa muda mrefu, ikiwa ni pamoja na ile ya mmojawapo wa Manaibu Waziri wa Wizara hiyo.

Mwezi Agosti, Rais alielekeza kwamba mapitio ya sheria za Fedha na Kanuni za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa yafanyike ili kuharakisha kushitakiwa kwa maofisa waliokula fedha za umma. Rais alisisitiza kutokubalika kwa zoezi lililozoeleka la kuwashitaki wale wanaohusika na ulaji wa fedha za umma kwa kuliita kosa la "mwenendo mbaya" badala ya kuliita "kosa la jinai" la ulaji wa fedha ya umma.

Tarehe 25 Mwezi Aprili, Mahakama Kuu ilipiga marufuku kisheria tabia ya takrima, utumiaji wa ukarimu, zawadi na upendeleo katika majimbo ya uchaguzi wakati wa kampeni za uchaguzi. Mahakama ilitoa uamuzi wake kwa kuihusisha na mashitaka yaliyofikishwa Mahakamani na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambayo ni Asasi isiyo ya Serikali ya hapa nchini dhidi ya tabia hiyo.

Wakati wa majadiliano kuhusu suala hilo mwaka 2005 na mapema mwaka huu, wanachama wa upinzani na wataalamu wa sheria walisema kwamba sheria inayoruhusu takrima ilikuwa inatoa "mwanya kwa ufisadi" na kupendelea chama tawala cha CCM, ambacho kilikuwa na uwezo mkubwa wa kufikia ruzuku nyingi za serikali.

Serikali iliendelea kutumia vyombo na wakala maalumu kupambana na ufisadi katika kipindi cha mwaka huu lakini nguvu zake za kuonyesha mabadiliko zilikuwa na mipaka. Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora kilipewa jukumu la kutekeleza sheria ya kupinga ufisadi, kuratibu jitihada za kupinga ufisadi na kukusanya taarifa kutoka wizara zote kwa ajili ya kuchapisha katika ripoti za kila mwaka. Hata hivyo Kitengo hiki cha watu watatu kiliendelea kwa kiasi kikubwa sana kutopata rasilimali za kutosha kukiwezesha kuendesha shughuli zake.

Kwa upande wa Bara Ofisi ya Kuzuia Ufisadi (PCB) ilikuwa na jukumu la kuchunguza kesi za ufisadi na kuzipeleka katika mahakama kwa mashitaka. Ofisi ya Kuzuia Ufisadi haikufanya kazi Zanzibar na iliendelea kuwa chini ya mamlaka ya Ofisi ya Rais, mambo ambayo yalikuwa kizuizi kwake kutoweza kukataa mashinikizo ya kisiasa na kushitaki kesi za ufisadi wa kiwango cha juu. Katika kipindi cha mwaka huu, Ofisi ya Kuzuia ufisadi iliendelea kupeleka kesi za ufisadi mkubwa kwa Mkurugenzi Mwendesha Mashtaka (DPP). Hata hivyo mashitaka ya kesi za ufisadi ziliendeshwa polepole na bila ufanisi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka ulioishia Desemba mwaka 2004, takriban asilimia 5 ya kesi za ufisadi zilikuwa zimesikilizwa katika Mahakama ya Sheria. Mwezi Novemba Rasi Kikwete aliteua Mkurugenzi Mkuu mpya wa Ofisi ya Kuzuia Ufisadi ambaye alionyesha kwamba Mkurugenzi Mwendesha Mashitaka aliendelea kupeleka takriban kesi mbili kati ya 10 katika mahakama kwa mashitaka.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Kuzuia Ufisadi; manung'uniko mengi yanayohusiana na ufisadi yalihusisha uchimbaji madini, masuala ya ardhi, nishati na uwekezaji. Mkurugenzi Mkuu mwishoni mwa mwaka alionyesha kwamba ofisi ya kuzuia ufisadi ilikuwa ikipeleleza kesi za ufisadi kwa asilimia 20 zaidi kuliko katika miaka ya nyuma zikiwa ni pamoja na kesi zilizodaiwa kuwa za ufisadi katika sekta ya umma.

Asasi Zisizo za Serikali ziliarifu kwamba madai mengi ya ufisadi yalihusu Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), maofisa wa serikali za Mitaa, Mamlaka za leseni, wafanyakazi wa hospitali na vyombo vya habari. Hapakuwa na kesi za kuwashitaki maofisa wa ngazi za juu wa serikali katika mwaka huu.

Kesi ya Ofisa Utawala Mkuu wa Tume ya Rais ya Usimamizi ya Pamoja ya Zanzibar aliyeshitakiwa kwa kosa la kula fedha za mfadhili mnamo mwaka 2004, iliendelea kusubiri uamuzi mnamo mwishoni mwa mwaka.

Mamlaka katika Visiwa vya Zanzibar ziliendelea kupinga jitihada za serikali ya Muungano kufungua ofisi ya sekretariati ya maadili katika Visiwa vya Zanzibar ili kuchuguza ufisadi huko. Ofisi moja ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwako Zanzibar lakini haikuwa na kibali kutoka kwa serikali ya Zanzibar kuchunguza kesi za ufisadi. Gazeti la Uingereza, *The Guardian* liliripoti tarehe 30 Desemba kwamba Baraza la Mawaziri la Zanzibar lilikataa kuweka saini kwenye muswada wa sheria ambao ungekuwa umeanzisha chombo cha kupigana na ufisadi; ungeanzisha Kanuni ya Maadili kwa viongozi wa Zanzibar, ungehitaji viongozi kutangaza utajiri wao ndani ya mwezi mmoja baada ya kuteuliwa au kuchaguliwa kushika madaraka na kupiga marufuku takrima Visiwani Zanzibar wakati wa uchaguzi. Makala hiyo ilimnukuu Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar akisema kwamba mawaziri walikuwa wameona kuwa mswada ulikuwa umeandaliwa vibaya.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo tayari ilikuwa na Ofisi Visiwani Zanzibar, ilipewa haki ya kufanya kazi huko katika kipindi cha mwaka huu (tazama sehemu ya 2.b).

Upatikanaji wa habari za serikali uliendelea kuwa mgumu sana. Marekebisho ya Katiba ya mwaka 2005 kuruhusu upatikanaji wa habari kwa umma hakika hayajabadili hali hii---- Sheria haitamki bayana habari za serikali. Maofisa wa serikali walikadiria kwamba asilimia 90 ya nyaraka zote za serikali, pamoja na fomu za utawala, zilikuwa za siri. Kwa mujibu wa mawakili wenye mamlaka ya kupata habari, sheria zinahusiana na usalama wa taifa, urushaji wa matangazo redioni, magazeti, magereza, maeneo yenye vizuizi, siri rasmi na polisi, ziliweka kizuizi umma usipate taarifa za serikali (tazama sehemu 2.a). Hapakuwa na utaratibu wa kukata rufaa kwa kutotoa habari, na

wananchi wengi waliendelea kupiga simu kwa ajili ya kutaka kupata marekebisho ya sheria hizi.

Bunge liliendelea kutumia Mfumo wa Habari za Bunge katika mtandao (POLIS) ili kuongeza upatikanaji wa taarifa za serikali. Hata hivyo ufikiaji wa POLIS uliendelea kuwa wenye mipaka, kwa vile ni wananchi takriban 300,000 tu kati ya wananchi milioni 37 wana mtandao wa Intaneti.

**Sehemu ya 4: Mtazamo wa Serikali kuhusu Uchunguzi wa Kimataifa na Uchunguzi Usio wa Kiserikali wa Madai ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu**

Aina nyingi mbalimbali za vikundi vya ndani ya nchi na vya Kimataifa kwa jumla vilifanya kazi bila kizuizi cha serikali vikichunguza na kuchapisha matokeo yao kuhusu kesi za haki za binadamu. Kwa jumla maofisa wa serikali walionyesha ushirikiano na mwitikio kwenye maoni ya AZISE. Hata hivyo, mashirika ya haki za binadamu yaliarifu kwamba viongozi hawakujibu au walikuwa wazito kuitikia maombi ya kutaka watoe taarifa. Inavyosemekana, Serikali ya Zanzibar iliziona AZISE kama wapinga serikali kwa hali zilivyo.

Ingawa Wabunge wengi walificha mioyoni mwao kukosa imani kuhusu AZISE bali kuamini kwamba zilikuwepo hasa kwa lengo la kukusanya fedha, mtazamo wao ulichangamka katika utawala wa Rais Kikwete, kutokana na maoni ya wachunguzi huru wa mambo. Wabunge wanawake waliitambua hasa shughuli za AZISE katika kutoa huduma zake katika umma. Spika mpya wa Bunge alizipa nafasi kubwa zaidi katika kipindi cha mwaka huu. Hata hivyo ushirikiano kati ya Wabunge na AZISE katika uundaji wa sera, ufuatiliaji na utoaji tathmini ya sera ya umma viliendelea kuwa dhaifu.

AZISE za hapa nchini zilizokuwa hai katika shughuli zilikuwa ni pamoja n Kituo cha Ukuzaji wa Haki za Binadamu, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Chama cha Waandishi wa habari Wanawake Tanzania na Chama cha Wanasheria Wanawake, Tanzania. Pia kulikuwa na AZISE ndogo zaidi zenye makao yake nje ya Dar es salaam. Kituo cha Huduma za Kisheria cha Zanzibar kilikuwa miongoni mwa mashirika machache hai ya haki za binadamu Visiwani Zanzibar. Mashirika yote haya yalikuwa huru – hayakujihusisha na serikali.

Wawakilishi wa serikali walikutana na AZISE zinazoshughulikia haki za binadamu na kushiriki katika semina za mafunzo katika mada zikiwa ni pamoja na sheria ya Ubinadamu ya Kimataifa, Ukeketaji wa sehemu za siri za wanawake, Ajira kwa watoto, Usafirishaji haramu wa binadamu na haki za wanawake.

Sheria ya AZISE ya mwaka 2002 ambayo haiihusu Zanzibar, inazitaka AZISE kujisajili katika kitengo cha uratibu wa AZISE

kilichoteuliwa na serikali katika Ofisi ya Rais. Kuanzia mwezi Februari 2005 mpaka Desemba mwaka 2006 zaidi ya AZISE 1,000 (baadhi zikiwa mpya na nyingine zilizokuwapo tayari) zilijisajili katika kitengo cha Uratibu wa AZISE kwa mujibu wa sheria hii.

Serikali ya Zanzibar pia ilisaidia baadhi ya shughuli za AZISE lakini ilikuwa na uvumilivu mdogo zaidi kwa zile asasi ambazo ziliikosoa serikali. Mbali na kurudia tena na tena maombi ya usajili, Asasi ya Mtandao wa ulinzi wa Kisheria wa Haki za Binadamu wa Afrika ilikuwa bado haijasajiliwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka.

Katika Bara, mnamo mwezi Aprili asasi ya elimu Isiyo ya Serikali ya Haki Elimu ambayo ilikuwa imezuiwa isichapishe makala au utafiti kuhusu shule ilianza tena shughuli kwa masharti yaliyowekwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Haki Elimu walikubali kwamba wasingetembelea shule tena au kuchapisha makala au utafiti kuhusu mfumo wa elimu nchini. Haki Elimu iliendelea na shughuli zake katika maeneo kama uteteaji uharakishaji wa uandishi wa habari za kipelelezi na uandaaji wa kijumuiya.

Hapakuwa na maendeleo ya upelelezi wa mauaji ya mwaka 2004 ya mfanyakazi mmoja wa Asasi Isiyo ya Serikali wilayani Ngara na washambuliaji wenye silaha, na hapakuwa na ripoti kwamba viongozi walikuwa wakifuatilia kesi hiyo (tazama sehemu 1.a)

Uhusiano baina ya serikali na shirika la UNHCR ambalo liliendelea kusimamia uendeshaji wa kambi 13 za wakimbizi za nchini, ulikuwa wa matatizo wakati mwingine (tazama sehemu 2.d). Shida moja iliyojitokeza wakati wa kipindi cha mwaka huu ilikuwa ni kufukuzwa kwa zaidi ya wahamiaji haramu kutoka sehemu ya Magharibi ya nchi ya Rwanda. Utambuaji miongoni mwa baadhi ya vyombo vya habari na umma ulikuwa kwamba wahamiaji hao waliofukuzwa walikuwa wakimbizi na hivyo kusababisha kuhusika kwa wakala wa misaada wa pande zote mbili za mpaka wa nchi mbili pamoja na shirika la UNHCR.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifanya kazi kwa uhuru bila kuingiliwa na serikali. Ilipata ushirikiano wa serikali Bara na ilipata haki ya kuwa hai Visiwani Zanzibar. Tume hiyo iliajiri zaidi ya watu 160 na ilifanya kazi kwa bajeti ya takriban milioni 2.4 (shilingi bilioni 3.1) ambalo ni ongezeko la $ milioni 2.1 (shilingi bilioni 2.7). Hata hivyo iliendelea kuwa na upungufu wa fedha, kukosa watumishi wa kutosha na kuelemewa na mzigo wa manung'uniko ambayo hayajaisha. Tume ilipokea manung'uniko ya nyongeza kutokana na kampeni za mwamko zilizofanywa kupitia vyombo vya habari. Kufikia tarehe 20 Juni tume ilipokea manung'uniko 14,487 na kutoa mapendekezo kwa serikali kuhusu manung'uniko 8,627. Tume iliainisha asilimia 1.8 ya manung'uniko kama

yanayohusiana na ukiukwaji wa haki za binadamu na mengi ya yale yaliyobaki yanahusiana na utawala usio sahihi wa serikali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka tume ilikuwa katika mchakato wa kutumia mfumo wa uendeshaji kesi kwa njia ya kompyuta ili kuboresha utaratibu.

Mwezi Septemba tume ilichapisha ripoti kuhusu hali ya magereza na kutoa kwa muhtasari mapendekezo kwa serikali kwa ajili ya uboreshaji (tazama sehemu 1.c).

Ingawa sheria ya mwaka 2001 iliyounda Tume hiyo ilitoa mamlaka kwa tume hiyo kufanya kazi Bara na Visiwani Zanzibar, viongozi wa Zanzibar waliizuia isifanye hivyo hadi marekebisho ya Bunge yalipopitishwa mwezi Oktoba (tazama sehemu ya 3).

Kamati ya Bunge ya masuala ya Katiba, sheria na utawala wa umma ina majukumu ya kutoa ripoti na kutoa mapendekezo kuhusu haki za binadamu. Idadi kubwa ya wajumbe wa Kamati walikuwa wakitoka katika chama tawala cha CCM, ikionyesha kuendelea kujihakikishia kupata wingi wa theluthi mbili za kura za wanachama. Hata hivyo kamati ilifanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa na serikali na athari za kisiasa na wachunguzi wa mambo waliiona kama chombo cha kuhakiki serikali.

Serikali iliendelea kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji wa Rwanda (ICTR) Mjini Arusha na serikali ilitoa msaada na ushirikiano wa ICTR.

## Sehemu ya 5: Ubaguzi, Utumiaji mbaya wa Sheria katika Jamii na Usafirishaji haramu wa Binadamu

Katiba inakataza ubaguzi kwa misingi ya utaifa, ukabila, upendeleo wa kisiasa, mbari au dini. Hata hivyo serikali haikutekeleza kikamilifu vizuizi hivi vyote daima. Ubaguzi kwa misingi ya jinsia, umri au ulemavu haikuzuiwa mahsusi na sheria lakini ilivunjwa nguvu hadharani katika matamko rasmi na kwa sera za serikali. Ubaguzi dhidi ya wanawake, wakimbizi, vikundi vidogo na waathirika wa VVU/UKIMWI uliendelea na migogoro ya ukabila katika jamii iliendelea kuwa tatizo katika baadhi ya sehemu za nchi.

### Wanawake

Ukiukwaji wa haki dhidi ya wanawake majumbani ulizidi kutapakaa. Sheria inazuia ushambuliaji lakini haizuii kinagaubaga shambulio baina ya wenzi wa ndoa. Mashinikizo ya kitamaduni, familia na kijamii mara nyingi ilizuia wanawake wasitoe taarifa za kushambuliwa na mara chache viongozi walichukua hatua dhidi ya wale walioshambulia wanawake kimwili. Mara nyingi polisi hawakukubali kufuatilia kesi za mashambulio ya ndani ya nyumba. Kwa mfano mwezi Desemba Agnes Mbuyamajuu, mwanamke aliyevumilia vipigo vikali vya mumewe kwa

zaidi ya miaka mitano, aliwaambia maripota kwamba vipigo hivyo vilihatarisha maisha yake, lakini kwamba polisi walikuwa hawajachukulia manung'uniko yake kwa makini.

Mila za jadi zinazowadhalililisha wanawake zilidumu kuwa na nguvu katika maeneo ya mijini na vijijini na wakati mwingine mahakimu katika maeneo ya vijijini walitetea vitendo hivyo. Ushambuliaji haukukomea katika mashambulio ya wenzi wa ndoa. Uchunguzi wa mwezi wa Aprili uliofanywa na Shirika la Afya ulimwenguni ulionyesha kwamba takriban asilimia 25 ya wanawake waliosaidiwa walipata kushambuliwa kimwili na wale ambao hawakuwa wenzi wao tangu wakiwa na umri wa miaka 15 na mmoja katika kila 10 walipata shambulio la kingono tangu wakiwa na umri wa miaka 15. Karibu mmoja katika kila 10 walisema walipata shambulio l kingono kabla hawajatimiza miaka 15.

Jamii iliiona tabia ya kumpiga mke kama kitendo kinachokubalika. Baadhi ya wanawake waliadhibiwa na waume zao kwa kutozaa. Mahakama zilitambua kwamba migogoro majumbani ni vyanzo vya talaka na wanawake waliohitaji ushauri kutoka kliniki za msaada wa kisheria upande wa Bara walitaja mara nyingi sana kwamba shambulio ndani ya nyumba ndiyo sababu ya kutaka kupata talaka. Kwa jumla wanawake walivumilia mashambulio ya ndani ya nyumba kwa muda mrefu kabla ya kutafuta talaka.

Mwezi Mei, Sooi Sadira, msichana wa miaka 12 wa Kijiji cha Saitsambu katika Wilaya ya Ngorongoro, aliuliwa na baba yake baada ya kukataa ndoa iliyokuwa imepangwa akaolewe na mzee wa miaka 30. Sadira alikaa na huyu mumewe mpya kwa usiku mmoja. Baada ya kubakwa alitoroka na kurudi kwao ambako baba yake alipanga kikosi cha vijana kumpiga kwa mzigo wa fimbo. Kwa mujibu wa Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, baba yake Sooi, Sadira Ole Karenmbu na mtuhumiwa mwingine Basilio Matei walikuwa bado hawajakamatwa. Mwezi Desemba AZISE mbili za hapa nchini zilipanga maandamano ya watu 300 ili kulaani mauaji hayo.

Sheria inatoa kifungo cha maisha kwa watu waliohukumiwa kwa kosa la kubaka. Hata hivyo, ubakaji uliendelea kuwa tatizo kubwa. Katika kipindi cha mwaka huu watu kadhaa walishitakiwa na wakahukumiwa kwa kosa la kubaka na shambulio katika sheria hii. Vurugu kwa misingi ya jinsi na jinsia ziliendelea kuwa tatizo katika kambi za wakimbizi (tazama sehemu ya 2.d)

Hakuna taarifa kuhusu ueneaji wa ubakaji zilizopatikana lakini ni takriban asilimia 5 tu ya kesi za ubakaji ndizo zilizopelekwa kusikilizwa mahakamani. Kwa mujibu wa Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar wakati mwingine kesi zilifutwa kwa sababu ya kukosa ushahidi. Inasemekana baadhi ya polisi waliwashauri wale waliobakwa wajisafishe kabla ya kwenda hospitali kwa uchunguzi, jambo ambalo lilichangia katika

kuondoa ushahidi muhimu. Katika kipindi cha mwaka huu kisiwa kikubwa cha Zanzibar, Unguja, kilikuwa na hospitali kubwa moja tu ambayo iliweza kufanya vipimo baada ya kubakwa. Hospitali hii ilikuwa hospitali ya binafsi na sheria inataka vipimo baada ya kubakwa vifanywe katika hospitali za serikali: Zaidi ya hayo, kwa kuwa waathiriwa wa kubakwa walipaswa kusubiri kwa muda mrefu hata kiasi cha siku sita kwa ajili ya uchunguzi, ushahidi mwingi wa muhimu ulipotea. Hospitali pekee ya serikali Kisiwani Pemba iliendelea na shughuli zake za kuchukua vipimo baada ya kubakwa mara moja kwa wiki. Inasemekana ubakaji na uonevu kijinsia kwa wasichana na wanawake wenye ulemavu vilienea katika kipindi cha mwaka huu.

Sheria inazuia ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike (FGM) ambayo pia hujulikana kama tohara. Hata hivyo desturi hii ilienea kiasi cha kutosha. Sheria inaelekeza kwamba yeyote aliyemfungia, anamlea au kumtunza msichana aliye chini ya umri wa miaka 18 na anayesababisha msichana huyo kukeketwa sehemu za uzazi, anatenda kosa la ukatili kwa watoto.

Ripoti moja ya Wizara ya Afya iliyotolewa mwezi Desemba ilionyesha kwamba asilimia ya wanawake na wasichana waliofanyiwa ukeketaji wa sehemu za uzazi (FGM) ilipungua kutoka asilimia 18 mnamo mwaka 1995 na kufikia asilimia 15 mnamo mwaka 2005. Data nyingine zilielekea kuonyesha kwamba wakati usambazaji wa utaratibu wa desturi hiyo ulikuwa ukipungua, umri wa wastani wa waathiriwa ulikuwa umepungua kufikia chini ya miaka 10 na kusemekana kuwa baadhi ya watoto wachanga waliozaliwa walikuwa wakikeketwa. Katika Mkoa wa Singida ukeketaji wa sehemu za uzazi mara nyingi ulikuwa ukifanywa kwa watoto wachanga waliposhikwa na Malaria au maradhi mengine ili athari nyingine zenye madhara kutokana na desturi hiyo zisingesababisha tuhuma miongoni mwa majirani na ndugu. Ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike ulikuwa ukifanywa na takriban makabila 20 kati ya makabila 130 ya hapa nchini na desturi hii ilikuwa imeenea sana katika mikoa 11 ya Bara ikiwemo Arusha, Singida, Kilimanjaro, Morogoro na Dar es salaam. Katika sehemu iliyobaki ya nchi, pungufu ya asilimia 5 ya watu waliendesha ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike (FGM). Njia inayotumika mara nyingi ni uondoaji wa kinembe ambayo ndiyo njia yenye maumivu kidogo zaidi ya ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike. Hata hivyo, ufyataji (ufungaji wa uke) ambayo ndiyo njia yenye maumivu makali zaidi pia ilitumika hasa katika kanda ya Nyanda za Juu za Kaskazini na Kanda ya Kati.

Adhabu dhidi ya desturi za ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike kwa wenye umri chini ya miaka 18 zilikuwa kati ya kifungo cha kati ya miaka mitano na 15, faini isiyozidi $ 235 (shilingi 30,000) au adhabu zote mbili. Kadhalika sheria inaruhusu ulipaji wa fidia kutoka kwa mkosaji kwenda kwa mtu aliyetendewa kosa hilo. Sheria haitamki kiwango cha chini cha

faini na pia haitoi ulinzi wa kisheria kwa wanawake wenye umri wa miaka 18 au zaidi. Wachunguzi wengi wa mambo waliamini kwamba ile sheria inalenga hasa wazazi au ndugu wa mwathiriwa; ilikuwa haikusudiwi kwa upana kuwalenga waliofanya kitendo hicho au ngariba walioajiriwa kukeketa sehemu za uzazi za kike (FGM).

Hapakuwa na ripoti za mashitaka zinazohusiana na ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike katika kipindi cha mwaka huu. hapakuwa na maendeleo zaidi kuhusu matukio mawili ya watu waliokamatwa na kushitakiwa kuhusiana na ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike yaliyofanywa mwaka 2005. Utekelezaji wa Sheria inayopinga ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike ulikuwa mgumu kutokana na sababu mbalimbali: Polisi wengi na jamii nyingi hawakujua kuwapo kwa sheria hiyo, polisi hawakuwa na vyanzo vya kufaa ili kulinda waathiriwa na mara nyingi waathiriwa walikuwa wakisita kuthibitisha dhidi ya wanafamilia wao na majirani ambao waliwalazimisha kufanyiwa ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike. Baadhi ya mashahidi waliogopa kulipizwa kisasi na wale waliopendelea ukeketaji huo.

Kadhalika ufisadi ulikuwa shida kutekeleza sheria ya kukataza ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike. Inasemekana baadhi ya wanakijiji walikuwa wamewapa viongozi wa pale fedha nyingi kiasi cha $ 235 (shilingi 300,000) ili waruhusiwe watoto wao watahiriwe bila hofu ya kukamatwa au kushitakiwa. Zaidi ya hayo mahakama zilifuta kesi nyingi kwa kisingizio cha kutokuwepo ushahidi, mara nyingi hata kama kulikuwa na ushahidi imara kutoka kwa waathiriwa na hata wazazi wao walezi wao au wale wanaoendesha vitendo hivyo kukiri.

Serikali iliendelea kutekeleza Mpango tekelezi wa Taifa wa 2001-15 wa kuzuia na kukomesha ukatili wa wanawake na watoto, mkakati ambao ulikuwa ni pamoja uondoaji wa ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike kwa kuwashirikisha wanaotenda vitendo hivyo, viongozi wa jamii, wanaume na wanawake. Vikundi vinavyopinga ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike viliwahimiza wabunge na maofisa wa serikali kuchukua nafasi kubwa zaidi katika utekelezaji ingawaje wabunge hawana mamlaka ya kulazimisha utekelezaji.

Katika kipindi cha mwaka huu serikali na AZISE ziliendelea kufanya maendeleo fulani katika kupunguza vitendo vya ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike. Katika kipindi cha mwaka huu vikundi vinavyopinga ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike viliendelea kuraghibisha mangariba kuhusu matokeo yenye madhara ya ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike na kuwapa mafunzo kwa ajili ya kazi zingine.

Upunguzaji wa desturi ya ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike uliendelelea kuwa mgumu kwa sababu baadhi ya maofisa wa serikali wa mkoa walipendelea au walinufaika kutokana na

desturi hiyo au waliogopa kuzungumza waziwazi kupinga vitendo hivyo kutokana na kutambua matokeo ya kisiasa ya kupinga ukeketaji na uwezo wa viongozi wa jadi waliounga mkono ukeketaji. Baadhi ya jumuiya zilizokuwa zikijua sheria inayopinga ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike ziliiona sheria hiyo kama tishio lisilo la haki kwenye mila ya utamaduni. Ukosekanaji wa taarifa ya tiba kuhusu madhara na athari za muda mrefu za ukeketaji uliendelea kuwa mgumu. Jumuiya nyingi ziliamini kwamba ukeketaji huongeza urutubishaji wa kupata mimba, hupunguza ashiki ya kutaka kufanya ngono ambayo husababisha umalaya na kupunguza vifo vya watoto wachanga. Kina baba wengi waliamini kwamba wangepata mahari kubwa zaidi kwa mabinti wao ambao wangekuwa wamekeketwa. Zaidi ya hayo, ngariba walitegemea ukeketaji kujipatia kipato.

Sheria inazuia umalaya. Hata hivyo, umalaya ikiwa ni pamoja na umalaya wa watoto wadogo uliendelea kuwa kitu cha kawaida. Wanawake maskini wa vijijini na wasichana wadogo waliohamia mijini walikuwa katika hatari kubwa zaidi. Mwaka 2005 kulikwa na ripoti kwamba wakimbizi wa kike walijihusisha katika umalaya. Katika kipindi cha mwaka huu hapakuwa na ripoti kuhusu tatizo hili.

Sheria inazuia bughudha za kijinsia kwa wanawake mahali pa kazi. Upana wa tatizo hili haukujulikana.

Sheria inatoa usawa kwa wanawake. Hata hivyo sheria za mirathi na ndoa hazizingatii wakati wote usawa kamili na katika hali halisi haki za wanawake hazikuheshimiwa. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto na Wizara ya Sheria zilikuwa na jukumu la kulinda haki za kisheria za wanawake. Ubaguzi dhidi ya wanawake ulikuwa mkubwa kabisa katika sehemu za vijijini ambako wanawake walitekelezwa katika kupima na kulea watoto na karibu hawakuwa na fursa kabisa ya kufanya kazi za ajira.

Sheria za uhamiaji za nchi hazitambui kwamba mwanaume anaweza kuwa tegemezi na hivyo kusababisha iwe vigumu kwa mme kutoka nchi ya kigeni wa mke ambaye ni raia kupata kibali cha kukaa nchini na kwa kuwa serikali haitambui uraia wa nchi mbili, mwanamke raia anayeolewa na mwanaume mgeni anaweza akapata shida ya kukaa kisheria nchini na katika hali halisi anaweza akalazimika kuachia uraia wake yeye mwenyewe. Tatizo hili lilikuwa likiongezeka katika kambi za wakimbizi kwa wanawake wa Kitanzania walioolewa na wanaume wa Kirundi ambao hawakuwa na sifa ya kupata vibali vya kukaa nchini kutokana na hali yao ya kuwa wakimbizi.

Sheria inatoa haki kwa watu binafsi kutumia, kuhamisha na kumiliki ardhi bila kujali jinsia na inatambua haki ya umiliki wa mwanamke. Wahamasishaji wa jamii waliarifu kuenea kwa

ubaguzi dhidi ya wanawake katika masuala kuhusu umiliki wa mali yanayohusiana na mirathi na talaka. Hili hasa ndilo lililokuwa tatizo Visiwani Zanzibar na maeneo fulanifulani ya Bara ambapo mahakimu walikubali utumiaji wa sheria ya Jadi au sheria ya Kiislamu. Wanawake ambao vyama vyao vilikuwa havijahalalishwa katika sheria za Jadi, Kihindu, Kiislamu, Kikristu au ndoa za kiserikali waliathirika sana walipotengana na wanandoa wenzao au wanandoa wenzao walipofariki. Zawadiel Mchome, Ofisa Tawala wa Mkoa wa Singida, alisema mwaka 2005 kwamba uporaji wa mali za wajane waliofiwa na waume lilikuwa limekuwa jambo la kawaida hapo mkoani.

Kwa mujibu wa Sheria ya Zanzibar, wanawake chini ya miaka 21 ambao hawakuolewa wanaopata mimba wanapaswa kupata adhabu ya kifungo cha miaka miwili (tazama sehemu 1.f).

AZISE kadhaa ziliendesha washa na semina na baadhi ziliendesha kliniki za msaada wa kisheria ambazo zilishughulikia masuala ya haki za wanawake yenye viwango mbalimbali.

**Watoto**

Katika mwaka huu Serikali iliendeleza azma yake kuhusu haki za watoto na ustawi wao. Serikali ilifanya jitihada halisi kushughulikia ustawi wa watoto ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa karibu na Mfuko wa Umoja wa Mataifa (UNECEF) na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa ili kuboresha ustawi wa watoto waliotelekezwa na takriban watoto yatima milioni mbili wa hapa nchini.

Sheria inaagiza kuwepo elimu ya lazima ya miaka saba, hadi kufikia miaka 15. Elimu ya msingi ilikuwa ya lazima, bure na kwa wote pote Bara na Zanzibar. Hata hivyo kulikuwa na idadi isiyotosha ya shule, vitabu na vifaa vingine vya elimu ili kukidhi mahitaji hayo.

Katika kipindi cha mwaka huu ada ziliendelea kutolewa kwa ajili ya kuandikishwa baada ya kidato cha pili, ambacho ni kiwango sawa na cha mwaka wa pili wa hatua ya juu ya sekondari. Matokeo yake baadhi ya watoto waliachwa bila kupata elimu ya sekondari. Hata hivyo, katika mwaka 2005 serikali ilipunguza ada kwa nusu na ilitoa ruzuku ili kutimiza ada iliyosalia kupitia Mpango wa Maendeleo ya Shule za Sekondari. Katika hali nyingi wazazi walipaswa kulipia vitabu, sare na chakula cha mchana na baadhi ya watoto hawakuweza kwenda shule kwa sababu walimu ambao hulipwa mishahara midogo sana walidai fedha ili kuwaandikisha au kwa sababu hapakuwa na ualimu.

Uwiano wa wavulana na wasichana katika shule za msingi na za Sekondari ulikuwa karibu unalingana. Wastani wa uandikishaji wa watoto katika shule za msingi ilikuwa ni asilimia 86 ambapo

asilimia 87 walikuwa wavulana na asilimia 85 walikuwa wasichana. Katika mikoa michache wastani wa uandikishaji shuleni kwa wasichana kwa kawaida ulishuka kwa kila mwaka uliongezeka hasa kwa sababu wasichana mara nyingi walipaswa kuwalea wadogo zao, kufanya kazi za nyumbani na kuolewa mapema, mara nyingi kwa amri ya wazazi wao. Desturi ya kulazimisha wasichana wanaopata mimba kuacha shule iliendelea. Wastani wa jumla wa kumaliza shule ulikuwa sawa kwa wavulana na wasichana yaani, asilimia 56 kwa shule za msingi na asilimia 33 kwa shule za sekondari.

Unajisi wa watoto uliendelea kuwa tatizo kubwa na kulikuwa na kutiwa hatiani kwingi katika kipindi cha mwaka huu. Watu wengi waliotiwa hatiani kwa kuwanajisi watoto walipewa adhabu ya mwisho ya kifungo cha miaka 30 jela.

Adhabu ya viboko shuleni lilikuwa tatizo. Mwezi Septemba mwalimu mmoja wa shule, Noel Namkumba wa shule ya Msingi Mtonya alikamatwa na kushitakiwa rasmi kwa kuwapiga viboko wanafunzi wawili na kuwapiga mateke, kuwapiga na kumng'oa meno ya mbele mtoto wa tatu. Utumiaji wa viboko uliendelea kupungua katika mwaka huu kufuatia jitihada za serikali za kuufikia umma, hasa Wizara ya Elimu na vyombo vya habari. Hata hivyo, Wizara ya Elimu ilisema mwezi Mei kwamba wanafunzi wenye kiburi katika shule za msingi na sekondari wangeendelea kuchapwa viboko kwa kuwa kupigwa viboko kunatajwa katika sheria. Waziri aliwaonya walimu wasiwapige wanafunzi ovyo na holela.

Ukeketaji wa sehemu za uzazi za kike (FGM) kwa wasichana (tazama sehemu ya 5, wanawake)

Kwa mujibu wa sheria, kujamiiana na mtoto chini ya miaka 18 kunachukuliwa kama ubakaji hata bila kujali ridhaa. Hata hivyo, sheria haikutekelezwa kwa dhati. Katika ukinzani wa wazi, sheria ya familia inawachukulia wasichana wa miaka 15 kuwa ni watu wazima kwa ajili ya kuolewa na kujamiiana. Ili kuweza kuolewa, msichana aliye na chini ya miaka 18 anahitaji apate ruhusa ya baba yake, mama yake au mlezi wake. Msichana yatima ambaye hana mlezi ambaye anataka kuolewa kwa umri wa miaka 15, 16 au 17 hahitaji kibali. Mahakama zilikuwa na hiari ya kuruhusu ndoa za wanandoa wenye umri wa miaka 14 iwapo zingeridhika kwamba yako mazingira maalumu ambazo zimesababisha ndoa hiyo ifungwe. Zaidi ya hayo, sheria inaruhusu wasichana wa kiafrika-kiasia kuolewa kwa umri mdogo wa miaka 12 alimradi katika ndoa hizo wanandoa wasikutane kimwili mpaka msichana afikie umri wa miaka 15.

Katika kipindi cha mwaka huu serikali iliendelea na jitihada zake za kutekeleza sheria hii kwa kumwadhibu mtu yeyote anayehusika kumpa mimba mwanafunzi msichana. Sheria inahesabu umalaya kwa watoto kama uhalifu. Hata hivyo utumiaji wa ngono

na usafirishaji haramu wa watu, ukiwemo wa watoto yalikuwa matatizo (tazama sehemu ya 5, Usafirishaji Haramu wa Watu).

Katika mikoa ya Iringa na Mbeya kulikuwa na ripoti watu waliokuwa wakifanya vitendo vya kichawi waliwaua watoto wa shule, kwa madai ya kuchukua na kuuza viungo vya mwili na ngozi. Katika mwaka 2005 kulikuwa na angalau na watu watatu waliotiwa hatiani kuhusiana na desturi hii.

**Ajira kwa watoto lilikuwa tatizo (tazama sehemu ya 6.d)**

Uuaji wa watoto wachanga uliendelea kuwa tatizo. Mwezi Juni maiti 22 za watoto ziligunduliwa katika mashimo ya takataka mjini Arusha. Polisi walipata ripoti za uchunguzi wa maiti zilizodhihirisha kwamba wale watoto wachanga walikufa kwa kukosa hewa. Mkuu wa Polisi wa Mkoa alisema ofisi yake ilikuwa imeahidi kufuatilia kwa makini wale waliohusika katika uuaji wa watoto wachanga. Katika kipindi cha mwaka huu hapakuwa na ripoti za mashitaka kwa kosa hili.

Idadi kubwa ya watoto yatima iliendelea kuwa tatizo. Mwaka 2005 Shirika la UNICEF lilikadiria kulikuwa na mayatima milioni mbili wengi wakiwa wametokana na janga la UKIMWI. Ripoti ya Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) iliyotolewa katika mwaka huu ilikadiria idadi hiyo kuwa milioni 2.5. Katika kambi za wakimbizi kwa kawaida watoto yatima walichukuliwa katika familia zingine na wale ambao hawakuchukuliwa, kwa kawaida walitazamwa kuwa watu ambao wangeweza kupatwa na shida kubwa na hivyo walipata msaada wa nyongeza na ushauri. Kulikuwa na idadi kubwa ya kutosha ya watoto wa mitaani pote katika miji ya Dar es salaam na Arusha. Watoto wa mitaani walikuwa na uwezekano mdogo sana wa kupata huduma za afya na elimu kwa sababu hawakuwa na mahali maalumu pa kukaa na fedha za kununulia dawa, sare za shule na vitabu. Kadhalika walikuwa na uwezekano wa kutumiwa vibaya kingono na watoto wa mitaani wakubwa zaidi au na watu wasio na kaya.

**Usafirishaji haramu wa Watu**

Sheria haikatazi usafirishaji wa aina zote na kulikuwa na ripoti kwamba nchi maana yake ni nchi ya asili, upitiaji na mahali waendako wanawake na wasichana wanaosafirishwa kiharamu kwa ajili ya kazi ya kulazimisha na utumiwaji mbaya kingono na kwa kiwango kidogo zaidi, wavulana wanaosafirishwa kiharamu kwa ajili ya kazi ya kulazimishwa. Waathiriwa walivutiwa na ahadi ya kipato kikubwa, fursa ya kupata shule na hali nzuri zaidi ya maisha hasa kutoka vijijini kwenda mijini.

Ilikuwa vigumu kupata idadi kwa namba tukio la usafirishaji katika kipindi cha mwaka huu, lakini desturi hii ilikuwapo katika mikoa mingi ya nchi. Waathiriwa wengi walisafirishwa

humuhumu ndani ya nchi. Wavulana walisafirishwa kwa ajili ya kazi ya kinyonyaji katika mashamba, migodini na katika sekta kubwa isiyo rasmi na hali wasichana kutoka vijijini walisafirishwa kiharamu kwenda mijini kwa kazi za ndani bila utashi wao. Wengi wa vijana hawa waliwatoroka waajiri waonevu na wakaingilia ukahaba wapate kuishi. Waathiriwa wengi walitoka katika mikoa ya Iringa, Mwanza, Dodoma, Kigoma, Dar es Salaam na Arusha. Inasemekana wasichana walisafirishwa kwenda Afrika Kusini, Saudi Arabia, Uingereza na inawezekana nchi nyingine za Ulaya kwa ajili ya kazi za ndani za kulazimishwa. Wanawake wa Kihindi--- walioingia nchini kisheria kufanya kazi kama wanamuziki, waimbaji na wacheza ngoma katika migahawa na klabu za usiku--- wakati mwingine walikuwa wakitumika kama makahaba baada ya kufika. Tarehe 4 Septemba, maofisa uhamiaji waliwafukuza wanawake watano wa kihindi mara tu baada ya kufika kwenye uwanja wa ndege wa Dar es Salaam kwa kushuku kwamba walikuwa wamekuja kufanya kazi kama wacheza ngoma kwa ajili ya klabu za Mujira. Kisiwani Zanzibar baadhi ya hoteli zilifadhili wasichana kwa ajili ya kazi ya hoteli ambao baadaye huwa wauza baa au makahaba. Hoteli zilitumiwa na wasafirishaji haramu kwa ajili ya shughuli za ukahaba.

Watoto wa familia za kipato kidogo walikuwa katika hatari kubwa ya kusafirishwa na wasichana ndio waliokuwa na uwezekano wa kufanyiwa hivyo kuliko wavulana kwa kuwa wasichana walitazamwa kuwa mzigo zaidi wa kiuchumi katika familia zao. Wasichana waliomaliza elimu ya msingi lakini hawakwenda shule za sekondari walikabiliwa zaidi na hatari hii. Kadhalika nchi ilikuwa ikiona ongezeko kubwa la kaya zilizokuwa zikiongozwa na watoto kadiri watu wazima zaidi walivyokuwa wakidondoka kwa sababu ya magonjwa yaliyohusiana na VVU/UKIMWI na vifo, huku wakiacha wategemezi wao wakikabiliwa na hatari ya ajira kwa watoto na usafirishwaji haramu.

Njia za usafirishwaji haramu zilitofautiana. Baadhi ya wasafirishwaji waliondoka makwao kwa msaada wa familia zao, baadhi kwa hiari yao ili kuepuka maisha ya vijijini na baadhi walisafirishwa na mtu fulani aliyekuwa amejitolea kuwasaidia kutafuta kazi za mjini za halali au haramu. Kulikuwa na ripoti kwamba wanaume waliwachukua wasichana wa vijijini waliokuwa wamemaliza elimu ya shule ya msingi lakini hawakujiunga na shule za sekondari. Wanaume hao waliwapa fedha wasichana hao na ajira na wakawaahidi wasichana hao maisha bora zaidi kama wangefuatana nao mijini. Hata hivyo, inasemekana wasichana hawa mwishoni waliishia katika umalaya au kazi za majumbani. Njia nyingine ya usafirishaji haramu ulihusu wazazi wenye kipato kidogo kuwakabidhi mtoto wao ndugu zao wenye hali nzuri zaidi ya kipato au watu wenye heshima katika jumuiya ambao walipewa jukumu la kumtuza mtoto huyo kama mmoja wa watoto wao. Baadhi ya watu walichukua fursa hii ya desturi ya jadi na kumweka mtoto katika hali ambayo alikuwa

katika hatari ya kutumika au kutendewa maovu. Wakati mwingine wakala wa kujitegemea wenye shughuli ndogondogo waliowachukua watoto kutoka vijijini waliandaa mahali pa kwenda na usafiri hadi majumbani.

Katiba ya nchi na sheria zinakataza kusafirisha haramu watu na zinatamka uwezekano wa kutoa adhabu ya kifungo cha kati ya miaka 10 na 20 au faini ya takriban kati ya $ 78 (shilingi 100,000) na $ 235 (shilingi 300,000). Wizara za Usalama wa Raia, Katiba na Sheria, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mambo ya Ndani zilishirikiana katika jukumu la kupiga vita usafirishaji haramu.

Hapakuwa na ripoti za mashitaka ya usafirishaji haramu katika kipindi cha mwaka huu. kulingana na Wizara ya Mambo ya Ndani, kulikuwa na ripoti za kesi mbili za usafirishaji haramu. Hapakupatikana habari zaidi kuhusu kesi hizi hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

Juhudi za serikali za utekelezaji wa vitendo dhidi ya usafirishaji haramu ziliendelea katika kipindi cha mwaka huu. Maofisa wengi walitambua maana za semi "Usafirishaji haramu wa watu" na "usafirishaji wa watu" na walikiri kwamba usafirishaji haramu wa watu lilikuwa tatizo. Viongozi walishiriki katika utafiti ulioendeshwa na shirika la Research International na kufadhiliwa na Shirika la Internatioanal Organization for Migration (IOM). Utafiti huo ulikuwa umeandaliwa ili kusaidia kujua kiwango na kina cha tatizo la usafirishaji haramu. Maofisa muhimu wachache wa Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Usalama wa Raia waliendelea na juhudi halisi za kuongeza mwamko wa umma kuhusu tatizo hili; kuhimiza kuwa na sheria makini zenye kufaa na kufuatilia mashitaka. Maofisa kadhaa walifanya mahojiano katika vyombo vya habari kuhusu suala hili.

Wizara ya Mambo ya Nje iliratibu Kamati ya ndani ya Wizara kuhusu usafirishaji haramu ambayo ilikutana mara tatu katika mwaka huu. Katika kipindi cha mwaka huu, Wizara ya Usalama wa Raia ilianzisha sehemu ya Kupambana na Usafirishaji haramu wa watu ndani ya sehemu ya Upelelezi wa Uhalifu. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; kwa msaada kutoka nje, waliandaa kijitabu cha mafunzo kwa wahudumu wa afya ambao wana mawasiliano ya moja kwa moja na waathiriwa wa usafirishaji haramu.

Kulikuwa na ripoti za hapa na pale kwamba baadhi ya maofisa wa polisi walikubali hongo ili kupuuza utendekaji wa ngono za kibiashara. Katika mwaka huu serikali iliendelea kujaribu kuwalinda waathiriwa wa usafirishaji haramu lakini rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya juhudi hiyo zilikuwa kidogo tu. Polisi wa hapa nchini na Maofisa wa Idara ya ustawi wa Jamii walibaini na kuwapeleka kwa hali ya kawaida waathiriwa wa usafirishaji haramu, kwenye AZISE ilizofanya kazi na watoto wa

mitaani na watoto makahaba, walipeleka misaada midogo ya chakula na vitu vingine kwenye Asasi hizi na walibainisha ardhi inayopatikana kwa ajili ya kujenga majengo mapya. Katika mwaka huu serikali na AZISE ziliendesha kampeni katika vyombo vya habari kuujulisha umma kuhusu hatari za usafirishaji haramu na serikali iliendelea na kampeni za mwamko wake kitaifa kuhusu aina mbaya kushinda zote za ajira kwa watoto kama vile ukahaba na kazi za majumbani za kulazimishwa.

Serikali ilifanya kazi vizuri na AZISE na ilikamilisha kazi ya shirika la IOM. Mnamo mwezi Juni Shirika la IOM liliendesha mafunzo ya saikolojia ya jamii kuhusu usafirishaji haramu na liliendesha semina ya siku mbili kwa waandishi wa habari mwezi Agosti kuhusu dhima ya vyombo vya habari katika kuzuia usafirishaji haramu wa watu. Shirika la IOM lilitengeneza na kusambaza vifaa kwaajili ya kuongeza mwamko dhidi ya usafirishaji haramu katika nchi nzima. Katika kipindi cha mwaka huu Wizara ya Kazi iliendesha semina kadhaa katika sehemu mbalimbali za nchi kuhusu ajira kwa watoto.

**Watu wenye Ulemavu**

Katiba inazuia ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu lakini hakuna sheria maalumu ya kutekeza kifungu hiki. Ingawa hapakuwa na ubaguzi rasmi dhidi ya watu wenye vilema lakini watu wenye vilema vya mwili waliwekewa vipingamizi vikubwa sana katika ajira, elimu, upataji wa huduma za afya na huduma nyingine za nchi kwa vikwazo vya miundombinu na ufinyu wa rasilimali katika bajeti. Serikali inaruhusu kuingia katika majengo yaliyo wazi kwa umma, usafiri au huduma za serikali kwa watu wenye ulemavu kupitia vifungu kadhaa vya sheria kama vile ile sheria inazingatia kuhakikisha kutotoa vibali kwa majengo ambayo hayana miundo ya majengo inayowawezesha walemavu kutumia. Hata hivyo ni majengo machache yaliyoweza kuingilika, si majengo yote yaliyohitaji vibali vya ujenzi na majengo mengi nchini yalijengwa kabla ya mwaka 1997 wakati agizo hili lilipopitishwa. Fedha za kurekebisha majengo yaliyopo hazikutolewa. Wizara za Elimu, Sheria na Kazi zilikuwa na jukumu la kutekeleza ulinzi na haki za watu wenye ulemavu katika elimu, madai ya kisheria, na haki za ajira kwa mpangilio huo. Idara ya ustawi wa Jamii ilikuwa na jukumu la kuratibu masuala ya ulemavu. AZISE chache za hapa nchini pia zilijaribu kuelezea taabu ya watu wenye ulemavu katika jamii. Rasilimali zilitolewa katika kipindi cha mwaka huu kwa ajili ya kupitia upya sheria zilizopo na taratibu zake katika eneo hili (tazama sehemu ya 1.e)

Kulingana na Asasi Isiyo ya Serikali ya Disabled Aids and General Engineering (DAGE), mabasi mengi ya abiria hayakusimama kwa ajili ya kuwachukua watu wenye ulemavu. DAGE

iliiomba serikali itafute njia za kusaidia jumuiya ya walemavu kuweza kwenda hukohuko kwa usalama na rahisi mijini.

Katika mwaka huu Wizara ya Elimu iliendelea kusaidia mfuko maalumu ulioanzishwa mwaka 2005 ili kuongeza upatikanaji wa elimu hasa kwa watu wenye ulemavu na watu wenye hitilafu nyingine katika jamii.

Kulikuwa na taarifa kwamba wanafunzi wenye ulemavu waliacha shule ambazo hazikuwa na huduma zao. Kwa mfano, familia za wanafunzi vipofu hazikuweza kuwapa karatasi ghali za breli na vinasa sauti.

Mwezi Septemba mwaka 2005 Wizara ya Elimu ilizuia Asasi moja Isiyo ya Serikali ya hapa nchini, Haki Elimu, isijishughulishe na au kuchapisha utafiti kuhusu shule za serikali. Katika moja ya matangazo kadhaa ya televisheni iliikosoa serikali, asasi hiyo ilisisitiza suala kwamba shule za serikali hazikuwa na vifaa vya kufaa kwa ajili ya wanafunzi wasioona na wanafunzi wasio na mikono au miguu (tazama sehemu ya 4). Serikali iliondoa kizuizi hicho mapema katika mwaka ule lakini ilibidi asasi ikubali kutoripoti masuala ya elimu siku za mbele.

Mwaka 2005 chama tawala cha CCM kilirekebisha ilani yake ya uchaguzi na kuongeza kiti cha nyongeza Bungeni kwa ajili ya walemavu na hivyo kufanya pawe na viti viwili viliyotengwa maalumu kwa ajili ya walemavu. CCM kiliamua kwamba kiti kimoja kama hicho kinapaswa kijazwe na mjumbe mmoja kutoka Zanzibar na kingine na mjumbe kutoka Bara.

Sheria inasema kwamba mpiga kura mwenye ulemavu kama vile kipofu anaweza akamwomba mtu atakayemteua yeye mwenyewe---mbali na watu wanaopigisha kura--- kumsaidia katika kupiga kura yake.

Kulikuwa na matukio ya kubakwa na kutendewa mambo maovu ya ngono wasichana na wanawake wenye vilema.

Desturi na imani za kitamaduni katika baadhi ya maeneo zilichangia katika fikra za ubaguzi miongoni mwa watu wenye vilema. Kwa mfano, Asasi Isiyo ya Serikali TRACED ilifichua kwamba familia moja Wilayani Mafinga katika Mkoa wa Iringa imekuwa ikimficha msichana mwenye ulemavu mbaya sana kwa miaka 15.

**Vikundi vidogo Kitaifa/Rangi na Kikabila**

Hapakuwa na sheria wala sera rasmi zilizowabagua Waasia au rangi nyingine yoyote. Hata hivyo, raia wengi wa Kiafrika waliona haifai kwa Waasia wapatao takriban milioni 1.5 nchini, ambao waliendelea kupata ubaguzi wa namna fulani. Raia wa

Kiasia walishika vyeo muhimu serikalini na walichaguliwa kuingia Bungeni. Maofisa wa vyeo vya juu serikalini waliendelea kusisitiza hadharani katika hafla mbalimbali ya kwamba wasingeweza kuvumilia hisia za kibaguzi au upendeleo wa namna yoyote. Hata hivyo hisia za umma kuhusu nafasi kubwa liliyo nayo kundi dogo la raia wenye asili ya Kiasia katika suala la uchumi, iliendelea kung'ang'aniwa. Mwaka 2005, kabla ya uchaguzi mkuu, vyama vidogo vitatu vya upinzani vilisisitiza kwamba endapo vingeshinda uchaguzi "vingerejesha" udhibiti wa utajiri wa taifa na rasilimali zake kutoka mikononi mwa wawekezaji wageni na raia wenye asili ya Kiasia na kuzigawa kwa raia wenye asili ya Kiafrika na Kiarabu ambao ndio, vyama hivyo vinavyoona, ni Watanzania wa kweli. Hata hivyo vyama hivi havikushinda kiti chochote na viongozi hawakufuata sera za kibaguzi.

Kulikuwa na matukio ya hapa na pale ya migogoro ya kikabila kuhusu ardhi au mifugo. Mwezi Septemba inasemekana kulitokea mapigano kati ya wafuaji na wakulima katika eneo la Mbarali yaliyosababisha kifo kimoja na kuacha majeruhi 12.

**Wenyeji wa Asili**

Wabarabaig na makundi mengine ya watu wanachama wa sehemu za Kaskazini waliendelea kudai fidia kwa ubaguzi wa serikali iliyopita, ambayo ni pamoja na jitihada za serikali kuwafanya wakubali kuchukua mtindo wa maisha ya kisasa na jitihada za kuwazuia waacha sehemu za malisho yao ambazo ziligeuzwa katika mashamba makubwa ya serikali ya ngano. Viongozi walitoa fidia kwa wenyeji wa asili waliokuwa wamepewa mahali pengine, lakini matatizo yalizidi kung'ang'aniwa.

**Uonevu na Ubaguzi mwingine wa Kijamii**

Usenge na usagaji ni makosa kisheria nchini Visiwani Zanzibar. Sheria imeweka adhabu ya kufikia hadi kifungo cha miaka 25 kwa wanaume wanaojiingiza katika vitendo vya kisenge na miaka saba kwa wanawake wanaojihusisha katika vitendo vya kisagaji. Hapakuwa na ripoti kwamba kuna aliyeadhibiwa na sheria hiyo katika kipindi cha mwaka huu.

Wasenge na wasagaji walikabiliwa na hatari ya kubaguliwa na jamii, hasa kwenye ngazi ya jumuiya. Mwezi Septemba Uamsho ilizuia mipango ya mgahawa mmoja ya kusherehekea siku ya kuzaliwa ya Freddie Mercury kwa kuwa mwanamuziki nyota huyo, mzaliwa wa Zanzibar alikuwa basha. Muungano wa Wabunge wa Tanzania dhidi ya UKIMWI ulizuia ubaguzi dhidi ya waathirika wa VVU/UKIMWI. Hata hivyo, kulikuwa na ripoti kwamba ubaguzi katika makazi, huduma za afya, elimu uliendelea kujitokeza dhidi ya watu takriban milioni 3.5 nchini wanaoishi na VVU/UKIMWI. Kulikuwa na ripoti hapa na pale kwamba waajiri

binafsi waliwafukuza au hawakuwaajiri watu kwa msingi kwamba walikuwa na VVU/UKIMWI. Serikali kwa kufanya kazi na AZISE, iliendelea kuuamsha umma kuhusu ubaguzi unaohusiana na VVU/UKIMWI na kuunda ulinzi wa haki za binadamu za wagonjwa wa VVU/UKIMWI. Mtandao wa wanasheria, waunda sera na madaktari waliendelea kuandaa jitihada na shughuli ingine za jinsi ya kushughulikia tatizo la kisheria, maadili na haki za binadamu linalohusiana na VVU na UKIMWI.

**Sehemu ya 6: Haki za Mfanyakazi**

**a. Haki ya Kuunganika**

Sheria inaruhusu wafanyakazi kuunda na kuingia katika vyama bila kupata kibali kwanza. Hata hivyo, katika hali halisi wajiri wengi katika sekta binafsi walichukua sera za kuwa dhidi ya vyama au kupata mbinu zilizopunguza haki hii. Waajiriwa waandamizi wanaweza wasijiunge na vyama vya wafanyakazi ambavyo pia vinawakilisha waajiriwa wa menejimenti wasio waandamizi.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka sheria ya kazi iliyopitishwa mwaka 2004 ilikuwa ikifanya kazi kiasi fulani tu ikiwa imeunda Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii. Jitihada za kuzindua Tume ya Usuluhishi na Upatanishi na Mahakama ya Kazi zilikuwa zimekaribia kukamilika. Hata hivyo Kanuni za Utekelezaji na Asasi zilikuwa bado zinaendelea.

Sheria ya mwaka 2004 ambayo inatumika Bara lakini haitumiki Zanzibar, inatambua haki za kuandaa chama za vyama vya wafanyakazi na imeanzisha utaratibu wa usajili wa vyama vya wafanyakazi vyama vya waajiri. Ni kile tu chama cha wafanyakazi kilichosajili zaidi ya asilimia 50 ya wafanyakazi pamoja wa mahali pale ndicho kinachoweza kujadiliana na mwajiri. Chama cha wafanyakazi au cha waajiri lazima kisajiliwe ndani ya miezi sita tangu kuanzishwa kwake na kushindwa kukisajili ni kosa la jinai kutegemeana na vikwazo vilivyowekwa na mahakama za chini.

Sheria za mwaka 2004 zimekusudia kuimarisha nguvu za msajili wa vyama (aliyeteuliwa na Waziri wa kazi) kurekebisha Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri na Mashirikisho. Inampa mwakilishi yeyote aliyeidhinishwa wa Chama cha Wafanyakazi kilichosajiliwa uwezo wa kuingia katika eneo la mwajiri na kuandikisha wanachama, kutegemea masharti yoyote ambayo ni ya maana na ya lazima katika kulinda maisha au mali au kuzuia kuvurugika kwa kazi. Mwajiri analazimika kufanya makato ya gharama za chama kama mfanyakazi atamruhusu kufanya hivyo. Iwapo mwajiri atashindwa kuwasilisha gharama hizo ndani ya siku saba baada ya kufanya makato, atatakiwa kulipa asilimia 5 zaidi kwa kila siku. Tawi la chama la nje linaweza kuanzishwa mahali pa kazi na wanachama 10 au zaidi wa chama cha

wafanyakazi na mwajiri analazimika kutoa livu kiasi cha kutosha kwa ajili ya wawakilishi wa chama cha wafanyakazi kuhudhuria mafunzo na shughuli na wajibu za maofisa wa chama cha wafanyakazi.

Serikali za Muungano na Zanzibar hazishiriki sheria zilezile za kazi na zinazitekeleza tofauti. Sheria ya kazi ya Bara inatumika kwa wafanyakazi wa sekta zote mbili: ya umma na ya binafsi. Sheria ya Bara inakitaka chama cha wafanyakazi kuwa na angalau wanachama 20.

Shirika la pekee la kazi, Umoja wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) ulikuwa na wanachama 317,000 mwaka 2005---pungufu ya asilimia 2 ya jumla ya wafanyakazi wapatao milioni 18. Takriban asilimia 27 ya wafanyakazi wote wanaohusika na kulipwa katika "sekta rasmi" ilikuwa ya kimuungano. Katika sekta ya kilimo ambayo ndiyo ilikuwa mwajiri mkubwa pekee, kiasi cha takriban asilimia 5 mpaka 8 ya idadi nzima ya wafanyakazi ilikuwa ya Kimuungano.

Kwa mujibu wa sheria hii chama cha wafanyakazi cha Bara kina haki ya kuwa na idadi ya wawakilishi ndani ya TUCTA kulingana na ukubwa wa idadi ya wanachama. Kwa vyama vyenye wanachama 100 au zaidi, idadi mahsusi ya wawakilishi, kutegemeana na ukubwa wa idadi ya wanachama, sharti wawe wanawake iwapo wanawake wameajiriwa hapo katika kitengo cha kazi.

Katika Bara sheria inazuia shughuli za kibaguzi za mwajiri dhidi ya wanachama. Hata hivyo, kulikuwa na ripoti kadhaa za kibaguzi za kupinga chama cha wafanyakazi katika sekta binafsi rasmi katika kipindi cha mwaka huu. Waajiri waliogundulika wakipinga shughuli za chama cha wafanyakazi walitakiwa kwa mujibu wa sheria hii kuwarudisha kazini wafanyakazi. Hata hivyo Tume ya Warioba ya mwaka 1996 ambayo ilianzishwa kutafiti ufisadi nchini, iligundua kwamba mara nyingi hongo ndizo zilizoamua iwapo mfanyakazi aliyefukuzwa katika kazi yake kweli alikuwa amerudishwa.

Vyama vingi vya wafanyakazi viliarifu kwamba waajiri wa sekta binafsi, hasa zile zilizokuja nchini kwa ubinafsishaji na mageuzi ya kiuchumi, zilifanya vitendo vya kibaguzi dhidi ya vyama vya wafanyakazi. Ingawa sheria ya mwaka 2004 ilizuia vitendo kama hivyo baadhi ya wawekezaji hawa inasemekana walitishia kuwafukuza au kuwapunguza kazi wafanyakazi waliotaka kuingia katika vyama vya wafanyakazi na baadhi ya waajiri hawakuruhusu kuitisha na kufanya mikutano ya kuajiri ndani ya mahali pao pa kazi.

Sheria ya kazi Visiwani Zanzibar inahusu wafanyakazi wa sekta binafsi tu. Wafanyakazi wa Zanzibar hawakuruhusiwa kujiunga katika vyama vya wafanyakazi vilivyoko Bara. Sheria ya Kazi ya Zanzibar inataka chama cha wafanyakazi chenye wafanyakazi

50 au zaidi kusajiliwa na pia kinaweka viwango vya kisomo kwa maofisa wa chama cha wafanyakazi.

Sheria ya kazi Visiwani haiwalindi wanachama dhidi ya ubaguzi wa vitendo vya kupinga chama, na kulikuwa na ripoti kadhaa za ubaguzi huo katika kipindi cha mwaka huu.

**b. Haki ya Kupanga na Kujadili kwa Pamoja**

Sheria hii inatoa fursa ya kujadiliana kwa pamoja, na wafanyakazi na wajiri waliitumia kwa uhuru katika kipindi cha mwaka huu. Hata hivyo, sheria haitumiki kwa sekta ya umma. Serikali ilitoa viwango vya ujira kiutawala kwa wafanyakazi wa serikali na mashirika yanayomilikiwa na serikali ambayo yana pungufu ya asilimia 5 ya idadi ya wafanyakazi wote.

Visiwani Zanzibar sheria inazuia migomo. Katika Bara wafanyakazi wana haki ya kisheria kugoma baada ya kuzingatia matakwa fulani ya kisheria na taratibu zenye kadhia ya usumbufu.

Katika Bara sheria ya awali iliendelea kuwa na nguvu ikisubiri utekelezaji wa sheria ya mwaka 2004. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Chama ambacho hakikuridhika na uamuzi wa mahakama ya kazi kinaweza kuendesha mgomo kisheria ikiwa, katika kura iliyopigwa mbele ya ofisa wa kazi wa serikali, idadi ya wanachama isiyopungua theluthi mbili ilichagua kufanya mgomo. Baadhi ya wachunguzi wa haki za wafanyakazi walisema masharti haya yalitumika kama kitisho cha kuwaogofya wanachama katika sekta ya umma. Taratibu za usuluhishi na upatanishi wa sheria ya awali zingeweza kurefusha mgogoro kwa miezi bila kuumaliza.

Katika Bara hapakuwa na sheria zinazokataza malipo dhidi ya wagomaji kisheria, lakini malipo hayakuwa tatizo.

Mbali na haki zilizotolewa katika sheria ya mwaka 2004, baadhi ya wachunguzi wa haki za wafanyakazi kama vile kituo cha Kisheria na Haki za Binadamu, walitoa maoni kwamba lugha katika sheria ya mwaka 2004 inaweza, katika hali halisi, kufanya migomo kuwe kugumu kwa wafanyakazi katika baadhi ya sekta. Sheria hiyo inapunguza haki ya kugoma ambapo kufanya hivyo kungehatarisha maisha na afya ya watu, upungufu ambao uliongeza kwa dhati takriban asilimia 50 ya idadi ya wafanyakazi waliochukuliwa kuwa "muhimu" na hivyo kutoruhusiwa kugoma. Wafanyakazi katika baadhi ya sekta (maji na majitaka, umeme, huduma za afya na huduma husianifu za maabara, uzimaji moto, udhibiti wa usafiri wa anga, mawasiliano ya masafa marefu ya usalama wa anga na huduma zozote za usafiri zinazotakiwa ili zitolewe) wamezuiwa wasigome na wafanyakazi katika sekta zingine wanaweza wakafikiriwa kuwa katika mkumbo huu wa kuzuiwa ama kwa muda au kwa kudumu baada ya utaratibu

unaohusisha uchunguzi, ilani, uwasilishaji, kusikilizwa kwa kesi na uchapishaji.

Visiwani Zanzibar ziko Kanda mbili za usindikaji wa Bidhaa za kupeleka Nje (EPZS) na tatu Bara. Ulinzi wa sheria ya kazi ulitumika kwa wafanyakazi wa kanda hizi (EPZS). Kwa Bara mazingira ya kazi katika kanda hizi za EPZS yalifanana na yale ya kwingineko. Hata hivyo, Visiwani Zanzibar kulikuwa na ripoti zisizothibitishwa kuhusu uonevu katika kazi.

**c. Ukatazaji wa Kazi za Kulazimishwa au za Lazima**

Sheria inakataza kazi za kulazimishwa au kazi za lazima, na Sheria ya Uhusiano wa Ajira na Kazi ya Mwaka 2004 inakataza mahususi kazi za kulazimishwa kwa watoto na ilifunga myanya katika amri ya kuipiga marufuku kikatiba ya kazi kama hiyo. Hata hivyo, kuna ripoti kwamba kazi za kulazimishwa na za lazima kwa watoto zilitokea (tazama sehemu za 5 na 6.d)

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2004 katika mgodi wa Dhahabu wa Geita, asilimia 85 ya wafanyakazi waliohojiwa waliarifu kwamba walilazimishwa kufanya kazi zaidi ya muda uliopangwa kwa kitisho cha kufukuzwa kazi.

Sheria inawaruhusu wafungwa kufanya kazi bila malipo kwenye miradi kama vile kilimo ndani ya gereza ili gereza liweze kujitegemea. Kadhalika wafungwa walitumiwa kufanya kazi ya kulazimishwa katika miradi iliyo nje ya gereza, kama vile utengenezaji wa barabara na miradi ya ujenzi ya serikali.

**d. Uzuiaji wa Ajira kwa Watoto na Umri wa chini wa Ajira**

Ajira kwa watoto liliendelea kuwa tatizo likiandamana na VVU/UKIMWI. Data kutoka 2000-01 (iliyoweza kupatikana ya hivi karibuni) ilionyesha kwamba asilimia 35.4 ya watoto wenye umri kati ya miaka 5 na 14 walikuwa wakifanya kazi. Sheria iliyopitishwa mwaka 2004 inaharamisha utumikaji vibaya wa watoto katika mahali pa kazi na inazuia kazi za kulazimisha au za lazima. Hata hivyo, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka utekelezaji wa kanuni na asasi kama vile Tume ya Usuluhishi haukuwa umeanza na hivyo kusababisha utekelezaji dhaifu wa vifungu vya ajira kwa watoto. Mwaka 2005 serikali iliajiri wakaguzi wa nyongeza ili kuboresha utekelezaji maana sheria ilianza kufanya kazi kikamilifu. Hata hivyo ajira kwa watoto liliendelea kuwa tatizo.

Ingawa utekelezaji uliendelea kuwa dhaifu, serikali ilitekeleza baadhi ya hatua ili kurahisisha tatizo ikiwa ni pamoja na kuongeza wakaguzi kadhaa wa kazi, kuhakikisha kwamba watoto wote wa umri wa kwenda shule wanakwenda shule, kuweka adhabu kwa wazazi ambao hawakuwaandikisha watoto wao shule na

kuwahamasisha waajiri katika sekta rasmi dhidi ya kuwaajiri watoto walio chini ya miaka kumi na minane.

Sheria inaweka umri wa miaka 14 kama umri mdogo wa mwisho kwa ajira ya mkataba na inasema kwamba watoto wanaweza kuajiriwa ili tu kufanya kazi nyepesi ambayo haielekei kuleta madhara kwenye afya na maendeleo yao na haiwakoseshi haki ya kwenda shule. Sheria inatamka kwamba watoto chini ya miaka 18 hawatafanya kazi melini au kuajiriwa mgodini, kiwandani au mahali pengine popote pa kazi ambapo mazingira ya kufanyia kazi yanaweza kuwa ya hatari, ikiwa ni pamoja na mahali pasipo rasmi na kilimo.

Sheria inatoa adhabu za makosa ya kuajiri watoto ikiwa ni pamoja na kazi za lazima, uonevu vinaweza kuwafaini isiyozidi $3,921 (Shilingi milioni 5), kifungo cha mwaka mmoja au vyote viwili. Hakuna adhabu iliyotolewa kwa mwaka wote.

Mwaka 2005 Shirika la ILO na UNICEF yaliripoti kwamba watoto walioondoka nyumbani kwenda kufanya kazi kama wafanyakazi wa ndani katika miji mingine au vijijini mara nyingi walilazimika kuingia katika biashara ya ngono. Kwa mujibu wa ripoti ya chama cha Conservation Hotel, Domestic and Allied Workers Union (CHODAWU) yaani Chama cha Muungano wa Wafanyakazi wa Mahotelini, Majumbani na Wafanyakazi walioshirikiana na Shirika la ILO, idadi kubwa ya watoto wafanyakazi wa majumbani walikuwa wasichana wengi kati ya umri wa miaka 13 na 15. Wengi wao walifanya kazi kati ya saa 12 na 14 kila siku, siku saba kwa wiki bila mapumziko au fidia ya ziada kwa saa nyingi zilizofanywa. Wakati mwingine walifanya kazi katika mazingira ya kunyanyaswa.

Shirika la ILO lilikadiria kwamba watoto kati ya 3,000 na 5,000 walikuwa wameajiriwa katika ajira ya majira katika mashamba ya biashara na wakati mwingine katika mazingira yenye hatari. Katika mikoa yenye migodi watoto kati ya 1,500 na 3,000 walifanya kazi katika migodi ya madini ya vito ambayo haikupimwa wakiwa wanajulikana kama watoto wa nyoka (snake boys) ambao walifanya kazi kwa baruti na kisha kutambaa katika mashimo membamba ili kusaidia kuweka vifaa vya kuchimbia madini. Kadhalika watoto walikutwa wakifanya kazi kama vile wavuvi, wahudumu wa baa, wachuuzi wa mitaani, waoshaji magari na wabebaji takataka. Pia walifanya kazi za nusu ufundi kama vile ufundi seremala na ufundi magari. Wasichana wenye umri mdogo kiasi cha miaka saba, na hata wavulana ambao wanazidi kuongezeka, walijihusisha katika ukahaba hapa nchini na wakati mwingine wakiwa wamesafirishwa kiharamu (tazama sehemu ya 5). Ajira kwa watoto ilikuwa imeenea sana visiwani Zanzibar. Watoto walitumiwa katika uvuvi, uvunjaji wa karafuu, kazi za majumbani, biashara ndogondogo kama vile kuuza keki, na biashara ya ngono karibu na vivutio vya watalii.

Wizara ya Kazi iliendelea kuwa yenye jukumu la uhimizaji wa kutekeleza sheria za Kazi bega kwa bega na Tume ya Usuluhishi na Upatanishi na Mahakama ya Kazi. Mwaka 2005 nyongeza ya maofisa 40 na wakaguzi waliajiriwa na kufunzwa na hivyo kukuza Jeshi la Ukaguzi wa Kazi la Taifa kufikia watu 145.

Kamati za Jumuiya, Kamati ndogo na Kamati za Wilaya za uratibu wa ajira kwa watoto zilibaini na kufuatilia kesi za ajira kwa watoto lakini zilifanya hivyo kwa viwango vilivyotofautiana vya ufanisi. Wawakilishi wa Mashirika ya ILO, UNICEF na AZISE za hapa nchini walihitimisha ya kwamba matatizo haya yalitokana na kukosekana kwa rasilimali na si kutokana na kukosa utashi wa siasa ili kupiga vita ajira kwa watoto.

Wizara kadhaa za serikali, ikiwemo Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo zina vitengo maalumu vya ajira kwa watoto, Serikali iliendelea kutekeleza, kwa kushirikiana na Shirika la ILO programu ya "Ndani ya muda Maalumu" kufuta aina mbaya zaidi ya ajira kwa watoto. Programu hii ilitaka kufuta ajira kwa watoto katika kilimo cha biashara, uchimbaji madini, kazi za majumbani na ukahaba katika wilaya 11 ifikapo mwaka 2010. Kwa msaada wa ILO, serikali katika programu ya "Ndani ya muda Maalumu" ilifuatilia idadi ya watoto waliozuiwa kuingia katika ajira mbaya sana kwa watoto na idadi iliyoondolewa katika ajira za namna hiyo katika wilaya 11. Kuanzia mwezi Januari mwaka 2002 mpaka mwezi Juni 2006, zaidi ya watoto 20,000 walizuiwa wasiingie, au waliondolewa katika ajira mbaya sana kwa watoto katika uchimbaji madini (2,081 walizuiwa na 1,466 kuondolewa), kazi za majumbani (3,292 walizuiwa na 2,701 kuondolewa), kilimo cha biashara (2,813 walizuiwa na 1,408 kuondolewa) na biashara ya ngono (2,992 walizuiwa na 4,045 kuondolewa). Idadi za sekta za uchimbaji madini na biashara ya ngono ilivuka lengo lililokuwa limewekwa katika nyanja hizo.

Kwa mfano, Umoja wa Afya na Maendeleo ya Wanawake wa Kiota (KIWOHEDE) Asasi moja Isiyo ya Serikali ikiwa inafanya kazi kama wakala wa utekelezaji ndani ya Awamu I ya programu ya "Ndani ya Muda Maalumu" ilijitolea kufanya shughuli za kuondoa na kuzuia ikiwa imelenga watoto wanaotumiwa katika biashara ya ngono. Kuanzia mwezi Januari mpaka mwezi Mei, KIWOHEDE ilizuia watoto 314 na kuondoa watoto 1,289 na hivyo kunusuru vizuri jumla ya watoto 1,603.

Chini ya Programu ya "Ndani ya Muda Maalumu" AZISE chache za hapa nchini, ikiwemo KIWOHEDE, ziliendelea kubaini na kuondoa watoto katika ajira mbaya na za kinyonyaji kwa watoto. KIWOHEDE ilifanya kazi kuwarekebisha wasichana waliokuwa wametumiwa vibaya wanaofanya kazi kama makahaba au watumishi wa majumbani. Shirika lingine, CHODAWU, lilianzisha ukaguzi kwa ngazi ya kijiji kubaini mifano ya ajira za kinyonyaji. Vilevile CHODAWU hushirikiana na kamati za ajira kwa watoto

ndani ya umma ili kuondoa watoto katika hali za kutumiwa vibaya.

**e. Hali Zinazokubalika za Kazi**

Mshahara wa chini kisheria kwa ajira zilizo katika sekta rasmi ulikuwa takriban $ 38 (shilingi 48,000) kwa mwezi. Hata baada ya kujaziliwa na marupurupu mengine kama pango, posho ya usafiri na ruzuku ya chakula, kima cha chini hakikuweza kumruhusu mfanyakazi na familia yake kupata kiwango kizuri cha maisha na hivyo wafanyakazi walitegemea ndugu wengine wa familia au ajira ya pili au ya tatu. Wafanyakazi wengi sana, hasa katika sekta isiyo rasmi inayoendelea kukua walilipwa chini ya kima cha chini cha mshahara. Kwa mfano inasemekana wafanyakazi wa majumbani walipata takriban $ 5.49 (shilingi 7,000) kwa mwezi.

Kulikuwa na ripoti kwamba ili kukwepa masharti ya kisheria kwamba inawabidi watoe marupurupu fulani na kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi walioajiriwa kwa zaidi ya miezi mitatu, waajiri walifanya desturi ya kuwafukuza wafanyakazi kabla kile kipindi cha miezi mitatu hakijaisha.

Hapakuwa na kipimo dhahiri cha kisheria cha wiki ya kazi kwa wafanyakazi wa sekta binafsi lakini waajiri wengi binafsi walizingatia wiki ya kazi ya siku sita yenye saa 44-48 za kazi. Kwa wafanyakazi wa serikali wiki ya kazi ilikuwa siku tano zenye saa 40 za kazi. Kwa jumla ilikuwa kinyume cha sheria kuajiri wanawake kufanya kazi kati ya saa 4.00 usiku na saa 12.00 asubuhi. Hata hivyo, waajiri mara nyingi walipuuza masharti katika kanuni hiyo.

Sheria kadhaa zinarekebisha usalama mahali pa kazi. Wizara ya Kazi, Vijana na Maendeleo ya Michezo iliendesha mfumo wa ukaguzi. Hata hivyo ufanisi wake ulikuwa mdogo. Viwango vya kazi havikutekelezwa katika sekta isiyo rasmi ambako asilimia kubwa ya wafanyakazi walikuwa wameajiriwa.

Wafanyakazi waliweza kumshitaki mwajiri kama mazingira yao ya kazi hayakupatana na viwango vya Wizara ya Kazi vya viwango vya afya na mazingira, kwa kupitia katika Chama cha Wafanyakazi, mfanyakazi anaweza kufungua madai ya ajira mbele ya ofisa wa kazi ambaye ataitisha majadiliano ambapo mwajiri na mwajiriwa kila mmoja atatoa maelezo yake. Mwajiriwa au mwajiri anaweza akakata rufaa kwa Waziri wa Kazi kuhusu uamuzi utakaokuwa umetolewa. Baadhi ya maofisa wa kazi walikubali hongo kutoka kwa waajiri ili kutokubali au kuthibitisha manung’uniko haya. Hapakuwa na ripoti kwamba wafanyakazi waliopeleka na kushinda manung’uniko kama hayo walikabiliwa na adhabu. Hata hivyo wafanyakazi hawakuwa na haki ya kujiondoa katika mazingira ya hatari bila kuhatarisha ajira zao kama wangepeleka manung’uniko na wakashindwa.